

UNAFASI YA DINI KATIKA JAMII YA KISASA KAMA
ILIVYOSAWIRIWA KATIKA RIWAYA ZA NGUVU YA SALA,
WALENISI NA BABU ALIPOFUFUKA 9

NA

[KARANJA, EDDAH, WANJA

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A)
KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

2005.


UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY



0271396 4

UNGAMO


Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.




KARANJA EDDAH WANJA

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii wa chuo kikuu.



DKT. T.M. OLALI



BW. H. M. MOGAMBI

TABARUKU

Tasnifu hii namtabarukia mpwa wangu mpendwa Leah Wambui Gicheru.

SHUKRANI

Mwanzo shukrani zangu ni kwa Chuo Kikuu cha Nairobi kwa kuyagharamia masomo yangu ya uzamili. Shukrani pia ziwaendee wasimamizi wangu Dkt. T.M Olali na Bw. H.M Mogambi ambao waliniongoza ipasavyo katika kuiandika tasnifu hii. Pokeeni shukrani zangu.

Shukrani nyingi pia kwa wahadhiri wangu katika Idara ya Isimu ambao ni mwenyekiti wa idara Dkt. Mbatia, Dkt. Mberia, Dkt. Kineene, Prof. Abdulaziz, Dkt. Buregeya, Bi. Njuguna, Bw. Mwangangi, Bw. Muungania na Bi. Mwaliwa. Ningependa pia kumshukuru Mwalimu T. Arege kwa usaidizi wake katika uanagenzi wangu chuoni.

Pia nawashukuru wazazi wangu, ndugu zangu, shangazi yangu Nancy, babu yangu na nyanya yangu ambao walinitia shime katika safari yangu ya masomo.

Shukrani pia ni kwa wanafunzi wenzangu tulioabiri jahazi hili la masomo pamoja. Hawa ni Lilian Gaki, Fridah Kaviti, mwalimu wangu Asumpta Matei, Wepoh Wesah, Kyalo Nguku, Julius Mungai, Wycliffe Were, Paul Mungai, Veronicah Maina, Vince Nyabunga, Rukia Swaleh, Mary Oichoe, Mediatrix Rapando, Njiru Kimunyi, Daniel Theuri pamoja na Nobert Basweti na Malanda M.

Pia nawashukuru marafiki zangu Bi. Kahuho, Bi. Mbuti, Bi. Muroko, Afisa Annastacia na Joyce kwa kunitia moyo nilipokuwa nikiandika kazi hii.

Siwezi pia nikasahau kuwashukuru Wanyonyi na Justus kwa kuichapisha kazi yangu. Kwenu nyote nasema ahsante na Jalia awajalie yote mema.

MUHTASARI

Katika kazi hii tumezihakiki riwaya za *Nguvu ya Sala* (1995) ya K.W. Wamitila, *Walenisi* (1998) ya K. Mkangi na *Babu Alipofufuka* (2003) ya S.A. Mohamed. Tumeangalia jinsi waandishi hawa wamelishughulikia swala la dini na kuonyesha nafasi yake katika jamii ya kisasa.

Uhakiki huu umegawanywa katika sura tano. Katika sura ya kwanza tumeelezea somo la utafiti, madhumuni, sababu za kulichagua somo hili, mipaka na upeo na yaliyoandikwa kuhusu swala la dini. Aidha tumeelezea misingi ya kinadharia iliyotumiwa katika utafiti huu. Pia tumeelezea njia tulizozitumia katika utafiti wetu.

Katika sura ya pili, tumeangalia jinsi dini ilivyosawiriwa katika riwaya ya *Nguvu ya Sala*. Tumeonyesha jinsi athari mbalimbali za dini zilivyojitokeza katika riwaya hasa katika kizazi kipya. Tumeonyesha jinsi wakati mwingine utamaduni wa wanajamii unavyopata ushindi ukilinganishwa na dini.

Katika sura ya tatu, tumeshughulikia dini katika riwaya ya *Walenisi*. Hapa tumeonyesha jinsi dini ilivyotumiwa na inavyotumiwa kuwalainisha na kuwadhulumu watu na kuwajaza kasumba ya maisha mema ya baadaye huko Peponi huku wakiteseka duniani.

Katika sura ya nne, tumechunguza dini katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* ambapo tumeonyesha jinsi ukengeushi unavyoweza kuwafanya wakwasi waidharau dini kiasi cha kujitoshanisha na miungu.

Sura ya tano ni hitimisho na mapendekezo.

YALIYOMO	UK.
Ungamo	i
Tabaruku	ii
Shukrani	iii
Muhtasari	iv

SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi	1
1.1 Tatizo la Utafiti	5
1.2 Madhumuni ya Utafiti	6
1.3 Sababu za Kuchagua Mada Hii	6
1.4 Mipaka na Upeo	9
1.5 Nadharia Tete	9
1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada Hii	10
1.7 Msingi wa Kinadharia	11
1.8 Njia za Utafiti	15

SURA YA PILI

2.0 Dini Katika Riwaya ya <i>Nguvu ya Sala</i>	16
2.1 Utangulizi	16
2.2 Udhanaishi Katika <i>Nguvu ya Sala</i>	16
2.3 Dini na Kizazi Kipya	20
2.4 Dini na Malezi ya Watoto	25

2.5 Dini na Utamaduni	29
2.6 Dini kama Imani Isiyo na Mashiko	32
Hitimisho	33

SURA YA TATU

3.0 Dini katika Riwaya ya <i>Walenisi</i>	34
3.1 Utangulizi	34
3.2 Dini na Dhuluma	34
3.3 Dini kama Utamaduni wa Kigeni	35
3.4 Dini na Siasa	38
3.5 Riwaya kama Kazi ya Kimbazi	44
3.6 Wigobezi katika Riwaya ya <i>Walenisi</i>	46
3.7 Riwaya ya <i>Walenisi</i> , Umaksi na Dini	48
3.8 Dini kama Suluhisho	52
3.9 Dini kama Imani Tatanishi	55
Hitimisho	57

SURA YA NNE

4.0 Dini Katika Riwaya ya <i>Babu Alipofufuka</i>	61
4.1 Utangulizi	61
4.2 Taswira ya Dini katika Riwaya	61
Hitimisho	70

SURA YA TANO

5.0 Hitimisho na Mapendekezo	72
5.1 Hitimisho	72
5.2 Mapendekezo	78
Marejeleo	80

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Tasnifu hii inahusu nafasi au umuhimu wa dini katika jamii ya kisasa kama ilivyojitokeza katika riwaya tatu: *Nguvu ya Sala, Walenisi na Babu Alipofufuka*. Tunatathmini jinsi waandishi wa riwaya hizi walivyoisawiri dini kama wanavyoiona katika jamii za kazi zao ambazo ni za Kiafrika. Tunaangalia jinsi dini inavyowaathiri binadamu katika nyanja na asasi mbalimbali za maisha yao kama vile siasa, elimu na kadhalika na kwa kufanya hivi kuona kama kweli ina umuhimu wowote au la.

Dini imeelezwa kwa fasiri mbalimbali. *Oxford Advanced Learners' Dictionary* (1998:988) inaelezea dini kama;

“Imani ya kuwoko kwa Mungu au miungu ambao wameuumba ulimwengu na kumjazia mwanadamu hali ya roho ambayo inaendelea kuwoko baada ya kufa kwa mwili.” (Tafsiri yetu).

Kwa hivyo, kulingana na kamusi hii binadamu huamini kuwa kuna Mungu au miungu waliouumba ulimwengu na pia wakaumba roho ya binadamu ambayo hata baada ya kufa kwake kimwili, ile roho haifi bali huendelea tu kuishi.

Coser (1963:276) anaelezea kuwa dini ni “...mkusanyiko wa imani, desturi na asasi ambazo binadamu katika jamii zote zinazojulikana wamezizua kama majibu kwa zile sehemu za maisha wanazohisi haziwezi kueleweka na kutawaliwa na akilirazini zao, na ambazo wamezipa maana inayojumlisha kurejelea kwa nguvu zisizoweza kuthibitishwa au zisizo za kawaida. Nguvu hizo

huhisiwa na waumini hawa kuwa zina athari muhimu kwa nafasi ya binadamu duniani na katika yale mambo yenye thamani ambayo huyapa maisha yake maana pamoja na ya wenzake.” (Tafsiri yetu).

Kulingana na maelezo haya ya Coser, binadamu huzua imani katika dini wakati anapokumbwa na mambo ambayo yeye mwenyewe hawezi kuyaelewa na basi anahisi kuwa lazima kuna nguvu zilizo juu yake ambazo zinaweza kuyaelewa mambo yale magumu. Binadamu basi huegemeza maisha yake yote na vyote vilivyo na thamani kwake na kwa wenzake katika nguvu hizo.

Pia tunaelezwa kuwa waumini wa dini zote hufasiri dini kama imani katika kiumbe au viumbe wenye nguvu zaidi kuliko waumini wenyewe kama inavyojitokeza katika vitabu vitakatifu kama vile *Bibilia Takatifu* ya Wakristo na *Qur'an Takatifu* ya Waisilamu.

Katika *Qur'an Takatifu*, tunaelezwa kuwa:

“Ni utakatifu kumwamini Allah, na Siku ya Kiyama, na Malaika na Vitabu.”

(Sura Al-Baqarah 2:177)

Kulingana na *Encyclopaedia of Seerah* juzuu 1:172 (katika Olali, 2004) *Qur'an* ndio muujiza mkubwa zaidi ambao Nabii Muhammad aliwapa wanadamu na hakuna mfano wake uliowahi kutolewa na mtu mwingine duniani. Kwa Waislamu, *Qur'an Takatifu* ni neno la Mungu, lililopokelewa kwa imani na kupitishwa na Nabii Muhammad. Uamilifu wake mkubwa ni kuwaongoza watu katika njia inayofaa.

Kulingana na *Encyclopaedia of Seerah* juzuu la IV: 43 *Qur'an Takatifu* haikuteremshwa chini mara moja bali ilikuja kulingana na mahitaji ya wanajamii wa Kiislamu katika kukabiliana na

matatizo mapya, kulingana na ukuzwaji wa maoni na dhana, na pia kulingana na changamoto geni zilizoikabili jamii ya Waislamu katika maisha yake halisi. Inaendelea kuelezea kuwa wakati wa kipindi cha Umakka, *Qur'an Takatifu* ilimwelezea mwanadamu siri ya kuwepo kwake na ya ulimwengu uliomzunguka. Ilimjulisha yeye ni nani, ametoka wapi, jukumu lake na kule ataenda mwishowe, ni nani aliyemtoa katika kutokuwepo hadi kuwepo, atarudi kwa nani na ni yapi yatakayomtendekaa mwishoni.

Mungu huwaahidi huruma wale wanaofuata maelekezo ya *Qur'an Takatifu*. Sura Al-Anam inasema kuwa:

“Na hiki ni kitabu kilichofunuliwa kama baraka, kwa hivyo kifuate na uwe mtakatifu ili upate huruma.” (6:155, katika Olali, 2004).

Qur'an Takatifu hujenga woga wa Mungu na uchaji na mapenzi kwake na basi kuwalinda waumini kutokana na maovu.

Kwa mujibu wa maelezo haya, Waislamu wanaamini kuwa Kiumbe aliye na nguvu kuwashinda ni Allah, Nabii wake ni Muhammad na Kitabu chake kitakatifu ni *Qur'an*.

Pia kuna fasiri mbalimbali za Mungu kama tunavyoelezwa katika kitabu cha Murdoch (1977:52) katika MacNamara, D. na Karmen, A.(wah.) (1983:163)anasema:

“Kuna yule Mungu asiye dosari wa Wakristo, yule mwenye mbeko lakini hana nguvu zote wa Wagiriki, na Yehova wa Waebrania wa kitabu cha Mwanzo aliyeumba kutoka kwa utupu.

Cha muhimu kutokana na fasiri hizi zote ni kwamba dini inahusishwa moja kwa moja na wanadamu na kwa hiyo ni asasi muhimu sana katika maisha ya binadamu. Imani na nguvu zote za wanadamu hutiwa kwenye dini na hasa kiumbe mwenye nguvu anayetegemewa na wafuasi wa dini hiyo. Kwa sababu hii basi, dini haiwezi kutenganishwa kamwe na binadamu na ndio maana ni vyema kushughulikia athari zake hasa kati ska fasihi ambapo waandishi wengi wameishughulikia kwa mitazamo mbalimbali, mingine ikiwa ni ya kukatisha tamaaa kama tutakavyoona katika kazi hii. Mingine kama ile ya Z. Burhani katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa* inaonyesha kuwa dini ina jukumu lake hasa katika maisha ya ndoa hasa kuidumisha kama asasi mojawapo muhimu katika jamii.

Kwa upande mwingine, tukiangalia dini za kitamaduni za Kiafrika, tunapata kuwa Waafrika waliamini kuwa kuna Mungu mmoja mkuu aliyeumba dunia na vyote vilivyomo. Wengi waliamini kuwa yeye huishi milimani na sehemu zao za kuabudu zilikuwa chini ya miti kama vile mikuyu na pia kwenye mapango. Hakukuwa na nyumba za ibada kama ilivyo sasa. Waafrika wengi pia hasa wale wa Afrika Magharibi waliamini kuwa kuna miungu wengine wengi mbali na yule mkuu, kwa mfano, mungu wa jua, upataji watoto, ulinzi, wa mito na wengineo. Mungu mkuu aliabudiwa tu katika jamii hizi walipohitaji kushinda katika vita fulani, katika uwindaji, wakati wa kiangazi na nyakati nyingine za matatizo. Haya ni kwa mujibu wa Gehman (1993).

Vile vile Waafrika hawakujenga nyumba za ibada kama zile za wazungu kwani waliamini kuwa Kiumbe wanayemuabudu ana uwezo mwingi sana na hivyo basi hangeweza kufungiwa ndani ya nyumba. (Nyaundi, 2003)

1.1 TATIZO LA UTAFITI

Katika kazi hii tumezihakiki riwaya tatu za *Walenisi*, yake Katama Mkangi, *Nguvu ya Sala*, yake K.W. Wamitila na *Babu Alipofufuka* yake S.A. Mohammed; kwa kuzingatia swala la dini au jinsi walivyoisawiri dini kuhusiana na nafasi yake katika jamii ya kisasa.

Kulingana na zile fasiri za dini tulizozichanganua hapo juu, tumepata jinsi dini huhusishwa na swala la maisha ya binadamu na kuonyesha jinsi mwanadamu alivyoitilia maanani na kuiweka kama ndio kithibiti cha maisha yake.

Kazi hizi za waandishi hawa ni za kisasa, zimeandikwa kati ya mwaka 1995 na 2001. Hawa ni waandishi ambao wameyaangalia maendeleo ya dini katika ulimwengu tunamoishi na kuona kuwa ni asasi muhimu na yenye athari kubwa, iwe nzuri au mbaya maishani mwa binadamu na hivi basi zimeimulika jamii ya kisasa jinsi ilivyo.

Tatizo la utafiti ni kuonyesha nafasi ya dini katika jamii ya kisasa kama inavyosawiriwa katika riwaya tatu za waandishi hawa watatu. Swali muhimu tunalolishughulikia ni: Je, dini ina umuhimu wowote katika maisha ya jamii ya kisasa au nafasi yake imepitwa na wakati na kudunishwa?

Tumezihakiki kazi hizi na kuona kama kweli bado dini ina umuhimu na nafasi sawa iliyokuwa nayo hapo awali na nyakati hizi za kisasa, au umuhimu huu umetupiliwa mbali na wanadamu kuanza kujithamini na kujitegemea wenyewe, kwa mfano, kwa kutumia elimu na ujuzi wao kama maulama.

Riwaya zote tatu zina mitazamo tofauti tofauti kuhusiana na dini na basi tumezishughulikia kandokando.

1.2 MADHUMUNI YA UTAFTI

Kusudi la kufanya utafiti huu ni kuonyesha jinsi wasanii hawa waratu wa kisasa wanavyosawia dini katika jamii ya kisasa.

Imani yoyote kuhusu dini huathiri maisha na matendo ya jamii pamoja na mtazamo wa maisha.

Tunakusudia basi kuonyesha nafasi ya dini katika maisha na matendo ya jamii kwa kurejelea riwaya za *Nguvu ya Sala* (1995), *Walenisi* (1998) na *Babu Alipofufuka* (2003).

Kila mmojawapo wa waandishi hawa ana falsafa yake kuhusiana na itikadi katika dini.

Tumeangalia jinsi walivyozifanyia tahakiki jamii walizozishugulikia katika kazi zao wakizingatia mitazamo na athari za dini katika maisha yazo.

Tumeonyesha jinsi mazingira mbalimbali ya Kiafrika hasa ya kiuchumi, kisiasa, uongozi, asasi ya familia na mengineyo yalivyoathiriwa na dini.

Pia tumeangalia mahusiano ya dini na mila na desturi za wanajamii na athari zake.

1.3 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII

Katika miaka ya hivi karibuni hasa karne iliyopita ya ishirini, waandishi wengi wamelishughulikia sana swala la dini. Dini ni asasi mojawapo muhimu katika jamii yoyote ile, tunapozingatia athari zake kwa wahusika mbalimbali katika jamii.

Waandishi, kama vile, E. Kezilahabi, K.K. Kahigi, M.M. Mulokozi, K.W. Wamitila, K. Mkangi na S.A. Mohammed wameshughulikia dini kwa mitazamo mbalimbali. Kezilahabi katika kazi zake zote za riwaya na ushairi ameshughulikia dini na kuonyesha jinsi inavyokatisha tamaa na hivyo haina maana yoyote kwa wanaojihusisha nayo. Kwa mfano, katika diwani yake ya

Kichomi, (1974:34-35) katika shairi la 'Nimechoka,' mwandishi ametumia taswira ya ratu anayening'inia chini huku ameshikilia waya ambayo inamkata vidole lakini hawezi kujinasua kwani hana nguvu zinazomzidi yule aliyeifunga waya ile.

Tunaambiwa:

Nilivyofikishwa hapo, na juu kupandishwa.

Na kwa hila gani, au, zilipofungwa

Ncha za waya hii ngumu ya maisha, sijui

Lakini najiona nimening'inia kama ndege

.....
Wanadamu wameinama. Wanasali kwa haraka sasa.

Utafikiri wanahesabu mchanga utakaojaza kaburi langu

Vichwa vyeupe vinacheka, kingine kinasema tena;

"Mnaliona hilo! Joga!" Vichwa vinacheka. Wanasali.

.....
Ninaendelea kuning'inia. Nimechoka. Mikono

Inauma; hatari ya vitimbo. Vinacheka. Wanasali

Sasa wanaimba. Sitaki nyimbo zao maana

Mimi bado nimening'inia na vitimbo having'oki.

Katika dondoo hii, ni dhahiri kuwa mwandishi anaelewa kuwa kuna Kiumbe mwenye nguvu aabudiwaye katika dini na anaonelea kuwa ndiye Muumba na ana uwezo wote juu ya maisha ya mwanadamu. Kiumbe huyu amemtupa binadamu katika ulimwengu katili na hawasaidii wanadamu kujinasua kutokana na mitego ya matatizo yao. Wanadamu wanashinda wakisali na kuimba lakini hawamsaidii mwenzao aliye katika matatizo kwani wao pia hawana uwezo juu ya Kiumbe yule anayemiliki maisha.

Kahigi na Mulokozi, katika diwani ya *Malenga wa Bara* wametoa maoni ya kukatisha tamaa kuhusiana na dini; katika shairi la 'Habari Mpya' tunaambiwa:

Kisha kijana mmoja pandikizi kasimama na kusema (na sauti yake ilisikika ng'ambo):

“Dini ni mia mzite wa uongo na maovu!
Ushirikina ulotia wengi makovu!
Gofu la taasisi linalojikongoja
Fikira na maendeleo ya mtu kufuja-
Yafaa kuchomwa moto! Kwani uwongo huu
Umeangamiza wengi! Wanaukumbata kwa kiruu
Unawapofusha, unawapumbaza, unawalemaza!
Wokovu wa mtu hautoki Mbinguni!
Wokovu wa mtu ni hapa duniani!
Vitisho vya jehanamu sikuze si hizi!
Siku hizi za zinduko na mapinduzi!
Nimesema! Majuto mjukuu humkuta
Mwongo ukweli asiyekamata!” (uk.109-110)

K.W. Wamitila ameonyesha jinsi watu wanavyoweza kuitumia dini vibaya pale wanapokumbwa na matatizo kama njia ya kujiliwaza, jinsi wahusika Richard na Mary walivyofanya katika *Nguvu ya Sala*. K. Mkangi ameonyesha jinsi wakoloni pamoja na wakoloni mamboleo huitumia dini kujinufaisha binafsi huku wakiwadhulumu walio wanyonge kwa kutumia jazanda ya Uchuna na Wachuna katika riwaya ya *Walenisi*.

S.A. Mohammed, katika *Babu Alipofufuka*, ameonyesha jinsi viongozi wengine wenye nguvu sana hujiona kama mungu (*Proteus*) na maisha yanapowageuka na kuwalemea basi wanamkasirikia na hata kumbeza Mungu kwa sababu ya hali zao mbaya.

Kutokana na maoni haya ya waandishi hawa miongoni mwa wengine, tunapata kuwa kuna tatizo linalotokana na kuhusiana moja kwa moja na dini. Tukizingatia kuwa hawa ni waandishi wa karne ya ishirini na ishirini na moja na wote ni wasomi tunapata kuwa wana tajriba kubwa katika maisha katika Afrika Mashariki, Bara la Afrika na ulimwengu wote kwa jumla. Wameona jinsi dini ilivyotumiwa na wakoloni kuwadhulumu na kuwatawala Waafrika. Wameona pia jinsi jamii

mbalimbali zilivyojihusisha na dini huku pia zikishughulikia tamaduni zao za kijadi. Wameonyesha mikengeuko ya wanajamii inavyoletwa na hali za kijamii na pia jinsi wengine wanaposoma sana hukosa imani katika dini.

Sababu yetu basi ya kuchagua mada hii ya utafiti ni kuonyesha jinsi waandishi, hasa hawa watatu, Katama Mkangi, S.A. Mohammed na K. Wamitila walivyoisawiri dini katika riwaya zao za *Walenisi*, *Babu Alipofufuka* na *Nguvu ya Sala* mtawalia. Kulingana na walivyoisawiri, ni dhahiri kuwa dini ina athari na nafasi kubwa katika jamii ya kisasa.

1.4 MIPAKA NA UPEO

Katika kazi hii tulijikita katika kuzihakiki riwaya hizi tatu za *Nguvu ya Sala* (1995), *Walenisi* (1998) na *Babu Alipofufuka* (2003).

Tuliyahakiki maudhui ya dini kama yalivyojitokeza katika riwaya hizi. Hatukuangalia swala la fani katika kazi hizi isipokuwa tu pale ambapo fani imeingiliana na somo letu.

1.5 NADHARIA TETE

Utafiti wetu uliongozwa na haipotesia hizi:

- Watu wengine huingilia dini wanapopatwa na matatizo
- Kuna watu ambao hutumia dini vibaya kwa kuwadhulumu wenzao.
- Baadhi ya watu hujiona kama mungu kwa sababu ya nguvu zao zilizokithiri kisiasa na kiuchumi.

1.6 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA HII

Sio mengi yaliyoandikwa kuhusiana na mada hii. Gatire, J.K. (1993) katika tasnifu yake ya uzamili ameshughulikia dini katika riwaya za E. Kezilahabi pekee. Wakati huo kazi tunazozishughulikia hazikuwa zimeandikwa.

Mungah, C.I (1999) katika tasnifu yake ya uzamili aliangalia dhana ya maisha katika novela mbili za Kezilahabi, *Nagona* na *Mzingile* na akashughulikia dini kwa kifupi pale inapohusishwa na maisha katika riwaya hizi mbili lakini hakugusia kazi tunazozirejelea.

Mwita, L.C, Andala, M., Mogambi, H. na Wamitila K.W. wameandika miongozo ya riwaya ya *Walenisi* na wameshughulikia swala la dini na athari zake kama mojawapo ya maudhui katika riwaya lakini hawakuzama ndani zaidi.

Kuhusu *Babu Alipofufuka*, Wamitila (2003) katika *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*, amegusia tu kuhusu kisaasili cha Kiyunani cha Proteus, 'mungu' wa baharini katika kuelezea tapo la Usasa na Usasaleo. Hakuzama ndani kuelezea mengi kuhusiana na mada yetu isipokuwa kusema tu kuwa kisaasili hiki kimetumika kufumbata 'ugeugeu' wa viongozi katika ngazi za kitaifa na kimataifa.

Kuhusu *Nguvu ya Sala*, Mbatia, A.M. katika Jarida la *Hekima* (2003:16) anasema kuwa kimsingi riwaya hii inauliza swali kuhusiana na nafasi au umuhimu wa dini katika jamii ya kisasa. Je, dini ina umuhimu wowote au nguvu ya sala ni jibu kwa kila jambo duniani?

1.7 MSINGI WA KINADHARIA

Katika kazi hii tunatumia nadharia mbili ambazo tunaona kuwa zinapatikana na mada yetu. Kuna nadharia ya Uhalisia. Uhalisia ni tapo la kifasihi ambako kazi za kifasihi zinachukuliwa kama zinazohifadhi au kuakisi sifa za kimsingi zinazohusishwa na uhalisi. Kazi zinazoangaliwa kama za kihalisia huwa kwa kiasi kikubwa, zimesawiri hali halisi ya maisha katika jamii-husika. Uhalisia hudumishwa kwa kutumia wahusika wa kawaida au wanaoweza kupatikana katika jamii halisi na kuyachunguza na kuyasimulia maisha yao na tajriba zao na kusawiri na kuonyesha mandhari na mazingira ya kawaida. Tapo hili liliwekewa msingi na mwanafalsafa Hegel, katika kitabu chake cha *Aesthetik*, (1820-9) alipendekeza matumizi ya neno hili kuelezea kazi ya kifasihi ambayo inauwasilisha ulimwengu wa maisha ya kijamii ambako kuna wahusika au mhusika anayetenda mambo kulingana na jinsi anavyochochewa waziwazi na hali aliyomo.

Usimulizi wake ni wa matukio kama yanavyotokea katika ulimwengu halisi au kwa maana inayokaribiana sana na hali iliyoko katika jamii. Mwandishi anapaswa kuyasawiri vilivyo maisha ya kijamii-kisiasa, kiuchumi na kitamaduni ya jamii-husika. Uhalisia husisitiza uwasilishaji wa maisha ya kijamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa. Waandishi wanaotumia tapo hili wanatarajiwa kutoa picha za wahusika, matukio na mandhari yanayooana kwa kiasi kikubwa na uhalisi wa jamii ya mwandishi anayehusika. Katika tapo hili hakupaswi kuwa na uajabu au fatansia ya aina yoyote, mandhari, mazingira na wahusika, vyote vinafaa kuwa halisi kama katika ulimwengu halisi. Picha na yaliyomo katika kazi hizi yanafaa kuwiana na ukweli na uhalisi wa jamii zinazohusika.

Nadharia ya pili ni ile ya Kimaksi ambayo inatambulishwa na ratazamo wa uhalisia, unaoonyesha mkubaliano fulani na kuegemezwa kwenye mawazo ya mwanafalsafa wa Kijerumani, Karl Marx (1818-1863). Umaksi unahusu nyanja mbalimbali kama vile uchumi, historia, jamii na mapinduzi. Msukumo wake mkubwa unawekewa msingi na kauli aliyoitamka Marx, akimzungumzia mwanafalasafa Feurbach kuwa 'wanafalasafa wameishia kuufasiri ulimwengu tu, lakini jambo muhimu ni kuubadilisha.' Mawazo haya pia yanapatikana katika Hoffman, J. (1975:26).

Hii ni falsafa ya kiyakinifu kwa vile inasisitiza hali za kiyakinifu za maisha kama vile mazingira ya kuishi kuliko mawazo katika maisha ya binadamu. Nadharia hii huuangalia uhailsi unaoonekana katika jamii.

Umaksi hueleza kuwa historia ya maisha ya binadamu inaweza kuelezeka kwa misingi yakinifu ya kiuchumi. Misingi hii huchunguza njia za uzalishaji mali pamoja na miundo ya kiuchumi inayoathiri uzalishaji mali hiyo na usambazaji wake. Swala hili linaunda kile kinachojulikana kama 'msingi' ambako ndiko kunakotegemezwa muundo wa juu au 'kiunzi'. Kiunzi ndicho kinachohusisha maadili, itikadi, dini, utamaduni na mengineo. (Wamitila, 2003 na Gehman, 1993)

Sifa za kiunzi zinaathiriwa kwa kiasi kikubwa na msingi, vile vile mabadiliko katika muundo wa kiunzi, kama vile, mageuzi katika muundo wa kiutawala, huweza kuathiri msingi. Karl Marx alisema kuwa historia ya maisha ya binadamu ni ya harakati za kitabaka. Katika *The German Ideology*, (1939:16) Marx na Engels walisema kuwa kitu cha msingi katika maisha ya binadamu

ni “kula na kunywa, kupata makazi, mavazi na mambo mengine mengi.”(Tafsiri yetu). Binadamu basi hutafuta nyenzo za kukidhi mahitaji haya na hufazimika kujiunga pamoja au kuunda umoja ili kuweza kuzalisha mali ya kukidhi haya mahitaji. Basi haya husababisha ugawaji wa majukumu au kazi na ndiyo msingi wa kuundwa kwa matabaka katika jamii hali ambayo huzua mfumo wa ubepari ambapo mali humilikiwa na wachache. Hawa hupata mali yao kwa unyonyaji wa umma na hasa wafanyikazi. Mfumo wa ubepari uendeleavyo ndivyo ubora wa kuzalisha mali unavyoongezeka na hivi kuimarisha tofauti za matabaka kwa vile wengine hufaidika kwa njia zisizo za haki. Unyonyaji huu, pamoja na mbegu za kujiangamiza zilizomo kwenye mfumo huu, vinachangia kuangusha mfumo wenyewe. Marx anaamini kuwa haya hutokana na mfanyiko wa kiasili wa kihistoria.

Wahakiki huamini kuwa ubepari kama njia ya uzalishaji mali utaangushwa na juhudi za wafanyikazi au wenyewe utaishia kujiangamiza kama tulivyodokeza hapo juu. Pia wanaona kuwa njia ya kusaidia maangamizo haya ni kudadisi, kukosoa, kushutumu, kulaumu na kufichua batili iliyopo katika itikadi ya kibwanyenye inayoimarisha ubepari. Hili ni jukumu muhimu la wanafasihi.

Umaksi pia huzungumzia ukengeushi ambapo Marx anasema kuwa ugawaji wa kazi husababisha utengano fulani kati ya binadamu. Mfumo wa kibepari unapoendelea kuboreka unaleta hali ya kuwa uhusiano kati ya mfanyikazi na tokeo la nguvu zake ni wa kitu kigeni. Watu wanaishia kukengeushwa na jamii yao kutokana na mfumo wa kiainisho unaosisitizwa na kukuzwa na ubepari.

Katika Umaksi pia, kuna 'ubidhaaishaji.' Marx alirejelea dhana ya 'bidhaa' kueleza kitu kinachozalishwa sio kutumiwa bali kubadilishwa katika mfumo wa kibepari wa soko. Bidhaa hutathminiwa sio kutokana na kazi yake bali kutokana na bei zinazoweza kuvuta. Sifa hii ya ubidhaaishaji inaishia kuwahuu binadamu ambao hawathaminiwi kama binadamu ila kutokana na uwezo wao wa kuzalisha mali. Dhana hii pia inaingiliana na ya Lukacs ya 'udude' inayorejelea hali ya kuwafanya binadamu sawa na vitu au kuwadhalilisha na kuwafanya vitu visivyokuwa na thamani.

Pia katika Umaksi kuna itikadi ambayo ni uwasilishi wa pamoja wa mawazo, fikra na tajriba hasa ikiwa vitalinganuliwa na uhalisi wa kiyakinifu vinakotegemezwa (Wamitila, 2003). Althusser, L. katika Wamitila (2003) anasema kuwa jamii za kitabaka hudumishwa na mwafaka unaozuliwa na ki-itikadi kwa njia mbili kuu; yaani, kwa matumizi ya Vyombo vya Ki-itikadi vya Dola na Vyombo Kandamizi vya Dola. Kwa mujibu wa Althusser, jamii za kitabaka hudumishwa kwa mkubaliano unaopatikana ki-itikadi kupitia kwa vyombo vya ki-itikadi vya Dola, kama vile, asasi za kielimu, sheria, siasa, mashirika ya wafanyikazi na jamaa au familia na vyombo hivi huchangizana na vile kandamizi vya Dola. Vyombo kandamizi hutumia nguvu ili kuwafanya watu hasa wafanyikazi kulitii tabaka tawala, kwa mfano, polisi, magereza na majeshi. Marx anaiweka fasihi katika uwanja mpana wa ki-itikadi pamoja na dini, falsafa, siasa, sheria, utamaduni, tathmini na sanaa kwa jumla. Fasihi huingiliana na uhalisia wa kijamii kwa vile inamulika mikinzano ya kijamii, kwa mfano, iliyosababisha mapinduzi ya Urusi, na pia fasihi huwasilisha miundo ya kiakili ya kikundi kinachohusika cha kijamii, hupinga hali fulani danganyifu katika jamii na aidha huhusisha lugha ambayo ni jambo muhimu katika jamii.

Nadharia hizi mbili, ya Uhalisia na ya Umaksi, zinaingiliana na yahiyo katika riwaya tatu tulizozishughulikia hasa kuhusiana na mada yetu inayohusu nafasi ya duni katika jamii ya kisasa kama inavyojitokeza katika riwaya hizo.

1.8 NJIA ZA UTAFITI

Kwa kiwango kikubwa kazi hii ilifanyiwa maktabani. Tulivisoma vitabu vingi vinavyohusika na kazi hii na pia kazi nyingine ambazo zilitusaidia katika utafiti wetu.

Pia tulivisoma vitabu vinavyoshughulikia nadharia tulizozitumia.

Tulivisoma pia vitabu vinavyohusiana na uhakiki wa kifasihi pamoja na kamusi mbalimbali.

Aidha tulitumia tasnifu mbalimbali zinazohusiana na kazi yetu hii.

Pia, kwa vile hawa ni waandishi wa Afrika Mashariki tumejaribu kutumia tajriba zao ambazo zinatawaliwa na hali ilivyo kimaisha katika eneo hili na hivi basi kuathiri uandishi wao. Hii ni kwa sababu tunaelewa kuwa uhusiano wa mwandishi na jamii, kufeli kwake au kufaulu kwake huathiri msimamo wake kuhusu maisha.

Pia tulitafuta ushauri na nasaha kutoka kwa maulama wa fasihi wakiwemo wasimamizi.

SURA YA PILI

2.0 DINI KATIKA RIWAYA YA NGUVU YA SALA

2.1 UTANGULIZI

Dini katika riwaya hii imesawiriwa kwa njia ya kukatisha tamaa. Mwandishi ameonyesha kutofaulu kwa dini katika nyanja zote za maisha ya wanajamii wa riwaya hii. Ameonyesha jinsi utamaduni wa jamii hiyo unavyofaulu ukilinganishwa na dini na hivi basi kuikejeli dini. Katika riwaya hii kuna mwelekeo wa kipengele cha udhanaishi kwa vile mwandishi anaonyesha ni kama kwamba maisha yanakoseshwa maana na dini.

2.2 UDHANAISHI KATIKA NGUVU YA SALA

Kulingana na *Oxford Advanced Learners' Dictionary* (1998:403) udhanaishi ni nadharia ya kuwa binadamu wana uhuru na wajibu kuhusiana na matendo yao katika ulimwengu usio na maana wala Mungu. (Tafsiri yetu)

Falsafa ya udhanaishi ilijitokeza Ujerumani miaka michache baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia na kuenea Ufaransa, Italia na nchi nyingine. Wanaoshikilia nadharia hii wanasema kuwa imani ya kuwoko kwa Mungu ni dhana isiyo na misingi yoyote. Wengine wanaona kuwa kuwoko au kutokuwoko kwa Mungu si suala la kuzua mjadala.

Ingawa wananadharia wa udhanaishi wana mitazamo na imani tofauti, kuna sifa mojawapo ya kimsingi, yaani kule kujishughulisha na swala la maisha ya binadamu hasa kwa kuisitiza uhuru wa binadamu na kutokubali kuwekwa chini ya mawazo ya kidhahania na asasi za kijamii zinaoudunisha.

Udhanaishi unabainisha uasi dhidi ya mawazo na asasi zinazozuia uhuru wa kibinafsi na kupuuzia uwajibikaji. Nadharia hii yanuia kumkombaa binadamu kutoka kwenye ulimwengu huu usiomjali kwa kumhimiza ajitegemee na kupigania uhuru wake kwa hali yoyote ile kutokana na nguvu zinazotaka kuuharibu-humfanya binadamu ajitambue yeye ni nani na kumwonyesha kuwa ana mamlaka juu ya matendo yake na kuwa anawajibika kwa kuendelea kuwoko kwake (Novack, 1960).

Pia, inashikilia kuwa hakuna kanuni, amri au mambo yaliyotangulia yanayowekea mipaka matendo ya mtu isipokuwa mtu mwenyewe aruhusu, kwa kuwa hatuwezi kuepuka kuchagua bila ya kuwa na uhakika-kwa madhara yetu wenyewe, ni lazima tuchukue msimamo wetu kwa ujasiri na kukabili matokeo yake.

Warnock (1970:123) anasema kuwa:

Tabia na matendo ya mtu kwa hivyo hutokana na jinsi (kutegemea mtazamo wake juu ya ulimwengu) anavyotathmini ulimwengu. Hakuna anayeweza kunilazimisha nikipe kitu thamani ya juu au chini (Tafsiri yetu).

Pia wananadharia hii wanasisitiza maisha yashughulikiwe kama yalivyo bila ya kutegemea nguvu zisizo za kawaida kwani hizi haziwezi kuwa kimbilio kutoka katika ulimwengu huu. Wanahimiza ubinadamu ueleweke katika hali halisi.

Dini inaangalia na kuelezea hali ya binadamu; maana ya maisha na furaha pamoja na hatima yake. Nadharia hii pia inazungumzia mambo haya kwa mtazamo tofauti.

Tukizingatia mawazo haya, tunapata kwamba mwandishi anataka kuonyesha kuwa maisha ya binadamu hayana maana yoyote na kuwa hawafai kuweka imani yao katika dini au kuitamini nguvu ya sala. Mwandishi ameonyesha jinsi dhiki, mateso na dhuluma zilivyozidi katika ulimwengu. Anausawiri umaskini uliopo hasa kwa kusawiri mtaa wa Kibera Laini Saba. Pia anaonyesha jinsi ukosefu wa ajira ulivyojaa kote na kuwadidimiza watu zaidi katika lindi ta umaskini. Aidha amesawiri uovu na dhuluma iliyopo katika kile kisa cha kijana mmoja aliyeuawa kikatili na fundi kwa kumpokonya mama mmoja kibogoshu ambacho hakikuwa na kitu chochote cha maana cha kugarimu maisha ya binadamu. Anamsawiri Richard kama mtu aliyekata tamaa kabisa; huyu anatafuta na kufanya kazi mbalimbali ambazo hazidumu bali zinamponyoka baada ya muda mfupi sana. Maisha ya mkewe Mary pia yamejaa usumbufu. Kwanza yeye hakumaliza masomo yake kwa ukosefu wa karo na alipopata kazi ya nyumba, bwana mwenye nyumba anamfanya kimada wake. Anaishia kupata mimba na kuiavya, anapokataa uhusiano na bwana huyo, anaambiwa kuwa atamfuta kazi na basi anaridhia tu. Mwishowe anapatwa na mke wa bwana huyo na kutimuliwa akiwa na mimba ambayo hangeweza kuiavya kwani shangazi yake mkristo hangemruhusu. Anapoolewa na Richard anachapwa na kuumizwa muda mfupi baada ya kuzaliwa kwa mwanao wa kwanza Susan. Mbatia, katika Jarida la *Hekima* (2003:17) anasema kuwa matatizo ya Susan yanasababishwa na jinsi ambavyo babake humlinda hivi kwamba hawezi kuhusiana na watoto wasio Wakristo na wavulana.

Tunapata kwamba Richard na Mary walijihusisha na dini pale ambapo walilemewa na dhiki na matatizo wasiyoweza kuyasuluhisha kwa nguvu zao wenyewe. Richard alifanya vibarua kadha lakini mwishowe alikuja kukosa hata kibarua cha siku moja na ndiposa alipomsikia yule mhubiri kule *Uhuru Park* aliamua kumpa Mungu maisha yake ili aone kama atapata suluhisho kwa matatizo yake ya ukosefu wa ajira na fedha. Mary, naye aliamua kumpa Mungu maisha yake ili

apate suluhisho kwa tatizo lake la kupata mimba nje ya ndoa. Mwishowe tunaona kwamba matatizo haya yao hayasuluhishwi kwani ukweli wa mimba ya Mary unajulikana, nayo majaribio ya Richard kuwa na jamii-kielelezo cha Ukristo hayafaulu kwani bintiye wa pili, Roselyn anapata mimba akiwa kidato cha pili.

Jinsi mwandishi alivyochukua mtazamo wa kidhanaishi, anakubaliana na wananadharia hii kuwa wanapendelea kubadilisha wasomaji wao na kuwafanya huru kutokana na mawazo yao ambayo hayakuwa na mashiko na kuwafanya sio tu wafikirie, bali pia waishi vingine (Warnock 1970: 7).

Katika riwaya hii kuna mambo yanayodhihirisha udhanaishi, mojawapo wa kipengele cha udhanaishi ni kuwa binadamu ni kiumbe kilichotupwa katika dunia isiyo na huruma ambamo anajaribu kutimiza malengo yake. Richard mhusika mkuu katika riwaya hii anathibitisha kipengele hiki cha udhanaishi. Yeye anasukwasukwa na dhoruba kali za maisha katika kutimiza malengo yake ya kuishi kama binadamu lakini hafaulu kamwe.

Vile vile kuna kipengele cha uhuru wa kila binadamu ambapo wananadharia ya udhanaishi wanasisitiza kuwa hakuna yeyote anayefaa kufanyiwa uamuzi maishani bali yeye ana uhuru wa kuchagua atakalo. Mwandishi amekubaliana na kipengele hiki kupitia mhusika Susan ambaye anapigania uhuru wake na wa wadogo zake kwa ukakamavu. Mwandishi, kupitia kwa Susan, anaonyesha kuwa kila mtu ana uhuru wa kuchagua ama kufuata au kutofuata imani hasa za kidini. Susan analeta afueni kwa dadake Roselyn aliyetimuliwa nyumbani na baba yao kwa kupata mimba akiwa shuleni. Hivi basi anafaulu kujinasua kutokana na udhibiti uliokithiri wa babake.

2.3 DINI NA KIZAZI KIPYA KATIKA NGUVU YA SALA

Katika riwaya hii vijana wamesawiriwa wakitichukulia dini kama usumbufu tu na ambayo haina manufaa yoyote kwao. Mwandishi ameonyesha jinsi vijana wanavyokuwa na mawazo yaliyo kinyume na dini na wanaweza kutenda lolote ili kutojijhusisha na dini pamoja na yote yanayohusiana nayo. Vijana wasomi nao hawaoni umuhimu wowote wa dini na wanaona ni kitu cha mapokezano kutoka jamii moja au kizazi kimoja hadi nyingine au kingine.

Tukiangalia idhibati kutoka kwenye riwaya yenyewe tunapata visa kadhaa kuhusiana na haya. Wakati Susan alipokuwa chuo kikuu katika mwaka wa kwanza, chumbani mwake mlikuwa na kijikaratasi ukutani kilichoandikwa:

*Christ is the Head of this
House
Unseen Guest at every
Meal
Silent listener to every
Conversation (uk. 147)*

Mmoja wa wanafunzi wa mwaka wa tatu katika chuo hicho alipotembelea chumba chake alikiona kikatatasi na kuzua mjadala:

“Unayaamini yale maneno?” aliuliza yue kijana.
Susan: “Nayaamini ndio.”
Kijana: “Umeokoka?”
Susan: “Mimi ni mkristo.”
Kijana: “Tangu ufike hapa university?”
Susan: “Hasha! Tangu siku nyingi tu.”
Kijana: “Una miaka mingapi tangu uwe mkristo?”
Susan: “Mbona unataka kujua hilo?”
Kijana: “Hamna sababu maalum.”
Susan: “Basi sioni umuhimu wake.”
Kijana: “Hapana ubaya kujua.”
Susan: “Wewe u mkristo?”
Kijana: “Huenda kanisa mara moja moja.”
Susan: “Unaamini kuwa Mungu yupo?”
Kijana: “Inawezekana akawapo.”
Susan: “Mwenyewe huamini?”

Kijana: “Huamini tu kwa kuwa ni imani ambayo nimeipata baada ya kukua. Inakuwa sehemu muhimu ya mapokezi yetu.”

Susan: “Imani katika Mungu haiwezi kuwa sehemu ya mapokezi yetu, huko ni kuidunisha mno.”

Kijana: “Lakini huoni mengi yaliyopo katika Biblia ni sehemu ya fasihi ya kimapokezi ya mataifa ya Mashariki ya Mbali.”

(Uk. 149 – 150) (msisitizo ni wetu).

Tukiangalia dondoo hii tunaona ya kwamba yule kijana haoni umuhimu wowote wa dini, kwenda kwake kanisani ni nadra, hata hana uhakika kama Mungu yupo au la, anaona kuwa imani katika dini ni fasihi ya kimapokezi ya mataifa ya Ulaya, kwa hivyo yeye haithamini dini kwa lolote lile na haya yanampa ujasiri wa kutoa mawazo kama yale yaliyo kinyume cha dini.

Mawazo ya Susan yanatodokezea pia kuwa vijana wasomi hawaithamini dini sana. Tunaambiwa:

“Nilishagundua kuwa wanafunzi wengi hawakuwa na imani dhati kuhusu dini. Sikuwa na budi ila kuwazoea tu, wengine niliwachukulia. Sikuona haja ya kujikalifu kuzigeuzania zao. Lazima nikiri kuwa uhalisi huu mpya ulishaanza kuitikisa kwa nguvu misingi ya imani yangu. Nilishaanza kuuona upungufu mkubwa uliokuwapo katika mwito wa baba kuhusu nguvu na satua ya sala. Lazima yalikuwapo mambo ambayo yalihatiji kukabiliwa kwa namna tofauti.”

(Uk. 150) (Msisitizo ni wetu).

Kutokana na maelezo haya tunapata kuwa wanafunzi pia waliitupilia mbali dini. Vilevile tunaona kuwa Susan naye, aliyekuwa na mashiko na imani thabiti katika dini ameanza kubadili mawazo yake kuhusu imani hii na nguvu ya sala. Wakati mmoja wakiwa katika shule ya upili, rafikiye Rose alipewa karatasi ya mtihani wa hisabati na mwalimu wao mtovu wa mbeko, Birundu, uliokuwa ufanywe siku iliyofuata, Susan anaikataa na kusema,

“Sheria ya Mungu inakataza”. (uk.97)

Wakati huo alitazama na kuhukumu kila kitu kwa mtazamo wa kidini, lakini katika dondoo iliyopo hapo juu, tunayaona mawazo yake yakibadilika kabisa na anasema kuwa alishaanza kuona upungufu mkubwa katika mwito wa babake wa nguvu ya sala, siyo mambo yote yangeenezeka na kutatuliwa kwa nguvu ya sala, ilibidi abadilishe mtazamo. Pia wakati dadake Roselyn alipopata mimba akiwa katika kidato cha pili, baba yao alimfukuza nyumbani na kwa kumtetea Susan anasema:

“Mtu hawezi kumtupa mwanawe kwa sababu ya imani tu; mwanzo hata siku hizi watu hawana imani kubwa na hiyo dini.”

na pia:

“Imani inayovunja mji haitufai.”

(Uk. 204, msisitizo wetu.)

Kulingana na maelezo haya ya Susan, ni dhahiri kuwa amebadilisha mtazamo wake kabisa kuhusiana na dini na kusema mambo ambayo hapo awali aliyaona ni kukufuru dini.

Pia kupitia kwa maswali yake ya balagha anapojiuliza:

“Niliuwazia mwito wake wa nguvu ya sala ambao aliukazania kwa muda mrefu. Je, ulikuwa wa kufaa au ulikuwa tasa? Je, matatizo mangapi ambayo yangesuluhishwa kwa mwito huo? Umaskini uliowavaa watu nchini kama Lubega, tofauti zilizokuwapo kati ya matajiri na maskini, udhalilishwaji wa wanawake katika jamii yetu. Nguvu ya sala?”

(Uk. 205, msisitizo wetu)

Kupitia kwa maswali haya ambayo ni ya kusisitiza tu maoni ya baadaye ya Susan kuhusu nguvu ya sala na dini, inadhihirika kuwa kwake yeye kama msomi, ameyadadisi mambo na kuhitimisha kuwa dini haina umuhimu au nafasi yoyote katika kizazi cha sasa.

Pia wakati Susan walikuwa wakizungumzia ile karatasi ya mtihani wa hisabati aliyopewa Rose na mwalimu Birundu, Susan alipoikataa na kusema kuwa sheria ya Mungu inakataa, Rose anamjibu;

“Watu waliivunja hiyo sheria uisemayo zamani gani...” (Uk.97).

Haya ni maoni ya Rose kama mmojawapo wa kizazi kipyua, kuwa watu hawaoni tena haja ya kuzifuata sheria za dini na basi, wamezivunjilia mbali wala hawazifuati.

Pia Richard, babake Susan alipokuwa katika kidato cha nne, yeye pamoja na vijana wenzake hawakuona umuhimu wowote wa dini, tunaambiwa:

“Alitanabahi kuwa ilikuwa zamani alipoenda kanisani, akiwa mwanafunzi wa kidato cha pili. Wakati huo alielewa wajibu wa binadamu kwa Muumba wake. La illahi. Hakutambua wajibu wake huo. Alielewa kanisa kama mahali pa makutano. Hapo ndipo alipokutana na marafiki zake mbalimbali; marafiki wa kike na kiume.

Alikumbuka walivyokuwa na mazoea ya kuketi sehemu ya nyuma kanisani. Sehemu hiyo ilikuwa na faragha ya kutosha. Waliweza kuongea kwa sauti ya chini bila ya kuwabughudhi waumini wengine. Mara kwa mara macho ya mhubiri yangewagundua. Mwanzo mwanzoni aliwakemea lakini baada ya muda ilimbidi awazoe. Yaelekea ndivyo ilivyokuwa jamii ya siku hizi; kizazi cha laana. Vijana wangeendelea kuongeaongea kwa sauti ya chini. Hatimaye wangeishia kutoka mmoja mmoja. Aghalabu huu ulikuwa wakati wa mahubiri, wengi wao walilalamikia mahubiri hayo: kuwa yalichukua kipindi kirefu.

Richard Ngunze alichukia mahubiri hayo: aliyachukia ghaya. Hakuwa na saburi ya kuyangojea; angewafuta wenzake wakitoka nje ya kanisa.” (uk.59).(msisitizo ni wetu)

Pia tunaambiwa kuwa:

“Hakuwa na mazoea ya kwenda kanisani kila Jumapili... Kuna siku moja tu ambapo asingekosa kwenda kanisani. Hii ilikuwa siku ya Krismasi. Wakati huo utaratibu ungebadilika. Wangepewa peremende. Kuna siku fulani wangebhatika kupewa soda kisha wangekumbushwa na wazee na wakuu wa kanisa kuwa walikuwa wakisherehekea siku ya kuzaliwa kwa Mkombozi wa ulimwengu. Vijana waliielewa siku hii kama siku ya peremende, biskuti na vipochopocho vingine. Sababu za kuwepo kwa peremende hizo na taanasa zilizoambatana nazo hazikuwashughulisha kamwe. Kuna wakati ilifika hadi ya vijana wa kijiji cha Misombe waliita Siku ya Krismasi, Siku ya Peremende. Sherehe za kuzaliwa kwa mtoto fulani katika zizi la ng’ombe huko ughaibuni hazikuwa na maana.”

(uk.60)

Kutokana na dondoo hizi, tunaona jinsi vijana, akiwemo Richard, walivyochukia mambo yote ya dini na walifurahia tu vijizawadi vilivyotolewa humo bila kujishughulisha na maana na umuhimu wa mambo hayo katika dini. Ingawa wazee na wakuu wa kanisa waliwakumbusha kuhusu kuzaliwa kwa Mkombozi wa ulimwengu kama kiini cha kusherehekea huko, haya hayakuwa na umuhimu wowote kwao. Hata Richard anapoamua kuingiliana na dini, haiwi kwa hiari bali ni ili kuondolewa tatizo alilokuwa nalo wakati ule la ukosefu wa ajira.

Mkewe Richard, Mary Kasiva, pia hakuona umuhimu wa dini katika ujana wake ila aliingiliana nayo ili apate suluhisho la tatizo lake la kuwa na mimba kabla ya kuolewa.

Pia, wakati Susan, Alexina na June walipohudhuria sherehe ya kuzaliwa kwa Cedric Mwambe aliyekuwa mhadhiri katika Chuo Kikuu walichokisomea, Cedric anapoulizwa na June kwa nini wengine huamini Mungu na Malaika huishi huko juu, anajibu:

“Ni vigumu kueleza lakini inawezekana ikawa imetokana na imani ya unyonge aliyonayo binadamu na ambayo inamfanya aamini kuwa nguvu zozote zinazomshinda ziko juu yake. Mungu yuko juu... kiongozi juu... mtawala juu.”

Huyu pia ni kijana na hivi basi mambo ya dini ni kizungumkuti kwake na kwa hivyo hayafuatili sana.

2.4 DINI NA MALEZI YA WATOTO

Katika jamii za Kiafrika watoto walichukuliwa kama waendelezaji wa familia walimozaliwa na walishikanisha wahenga waliokufa na wale watu walio hai. Watoto walimilikiwa sio tu na wazazi wao, bali pia na jamaa wote wanaohusiana nao kinasaba. Mara nyingi watoto walitumwa kuishi na jamaa zao wa mbali bila ya wazazi wao kuwa na tashwishi yoyote kuhusiana na malezi yao. Watoto walikuwa ishara ya baraka za Mungu na pia walikuwa na thamani kwani wangesaidia katika kazi za nyumbani. Kijadi watoto walilelewa na jamaa wote, wangesahihishwa na kuadhibiwa na mtu yeyote mzima pindi watendapo maovu. Watu wazima pia walikuwa na mamlaka ya kuwapa watoto majukumu rahisi. Babu na nyanya pia walikuwa na jukumu la kuwalea watoto, waliwafundisha kuhusu mahusiano ya mume na mke na majukumu, maadili na desturi za kijamii. Kwa kiwango kikubwa waliwatambia watoto hadithi, kuwatolea methali na nyimbo katika mafunzo yao. Watoto wakubwa pia walihusika katika malezi ya ndugu zao wadogo. Hawa wakubwa wakati mwingine walikuwa na mamlaka sawa na ya wazazi wao juu ya wadogo zao.

Wazazi nao walikuwa na jukumu kubwa la kuwafundisha watoto majukumu ya kiutu-uzima hasa katika ugawaji wa kazi za kinyumbani. Baada ya umri wa miaka minane au kumi, watoto wengi walijifundisha majukumu yao ya kikazi kwa kutenda kazi pamoja na mzazi wa jinsia moja nao.

Kwa hivyo, wavulana walipitisha muda mwingi wa saa za kazi zao na baba zao na wasichana na mama zao. Lilikuwa pia ni jukumu la wazazi kuhakikisha kuwa watoto walikua wakiwa na tabia na mienendo inayofaa. (D. Kayongo-Male na P. Onyango 1991: 7, 19-20).

Ukristo ulienea katika maeneo mengi ya Afrika wakati wa ukoloni. Makundi mengine ya Kikristo yalihimiza ubinafsi kwa kutumia njia kama vile kuwahimiza wazazi wachukue udhibiti wa kibinafsi wa ufundishaji wa mbeko kwa watoto wao kuliko kutegemea sana jamaa zao wengi. (khj: 47).

Malezi ya watoto hasa wa viongozi wa dini yanaelekezwa tu na imani zao katika dini. Mwanzoni mwa riwaya tunaona Susan, mwanawe Richard, akichapwa na babake kwa sababu ya kucheza na watoto wa jirani yao. Hakuna sababu mwafaka inayotolewa isipokuwa kwamba watoto hao si wakristo ingawa tunaenezwa kuwa walienda kanisani. Kipigo hiki kilifanya familia hii ya Richard kulala njaa. Susan anajiuliza maswali kadhaa baada ya kipigo hicho.

Tunaambiwa:

“Mimi nilijitahidi sana; labda ufalme aliouzungumzia baba ulikuwa muhimu kuliko chakula. Sikuacha kushangaa ikiwa Mungu alikuwa mkali kama alivyokuwa baba. Je, alifoka kwa hasira kama alivyofanya baba? Je, aliwalaza watu njaa?”

Pia baada ya mtihani wa darasa la nane, Susan alichapwa na babake kwa sababu ya kufuatana na wenzake matembezini. Roselyn anapopata mimba akiwa kidato cha pili anapigwa na kufukuzwa nyumbani na babake. Richard aliyafanya haya yote kwa sababu alitaka jamii yake iwe kielelezo chema kwa watu wengine wote hasa kwa vile alikuwa mchungaji wa kanisa.

Wazazi waliojijhusisha zaidi na dini hawawapei watoto wao mawaidha ya kimaisha. Wanawafanya tu kukariri vifungu virefu vya Biblia. Jambo hili haliwapendezi watoto wengine, kwa mfano, Bethsheba mtoto wa baba mkristo, baada ya kumaliza masomo ya shule ya msingi anasema atatamani kwenda shule ya bwani ili ayakwepe mafundisho ya lazima ya Biblia kutoka kwa babake. (uk 20)

Susan anapokwenda shule ya upili, mawaidha anayopewa na wazazi wake tu ni kuwa:

“Jitunze vizuri mwanangu; usiniaibishe mimi,” alisema baba.

“Mm! Mwanangu jitahidi usimwaibishe babako,” alisisitiza mama.

“Kumbuka utapambana na majaribu ya kila aina mwanangu,” alisema baba.

“Kumbuka uwezo wa maombi,” alisema mama. Kabla hajamaliza alikatizwa kauli na baba.

“Usisahau nguvu ya sala.”

“Mwili wako ni kanisa la Bwana,” alisema mama.

“Litakase kanisa hilo,” alisisitiza baba.

“Amina, mwanangu usikubali kurengwa na marafiki wabaya,” alishauri mama.

“Zikemee hila za mwovu,” alichangia baba.

“Kumbuka u mtoto wa nyumba ya kikristo,” alinikumbusha mama.

“Kuwa kielelezo kizuri, kumbuka jamii nzima imenikodolea mambo mimi babako,” alimalizia baba.

Katika mashauri haya hakuna lolote linalohusiana na jinsi ya kuishi maisha halisi mbali na yanayotakikana katika dini. Anasisitiziwa tu nguvu ya sala. Malezi ya aina hii yanaonyeshwa

jinsi yanavyofeli pale ambapo Roselyn anapata mimba kwa kukosa maelekezo ya maisha halisi isipokuwa tu nguvu ya sala.

Susan anapomkosoa babake kwa kumfukuza Roselyn anasema:

“Kama kuna makosa yoyote yamo katika malezi mliyotupa. Mmekazania tuyafuate mafundisho ya Biblia bila kutuelekeza katika maisha halisi ya ulimwengu huu.” (uk.202)

Mamake anapomuuliza kama mafundisho ya Biblia ni mabaya, Susan anajibu:

“Sio mabaya lakini kuna na mambo mengine na ndio maana Roselyn akatumbukia katika mtego huu.” (uk.202)

Kwa hivyo mwandishi kupitia kwa mhusika Susan anataka kusisitiza kuwa malezi yanayowekewa misingi katika dini tu hayafai kwani hayawapi watoto mwelekeo unaofaa katika maisha halisi.

Bethsheba pia aliishia kuolewa baada tu ya kidato cha nne na hamna cha kujivunia isipokuwa usumbufu mtupu kwani hakuwa ameelekezwa na wazazi wake kuhusu uhalisi wa maisha ya ndoa.

Hapa basi mwandishi ameonyesha dhahiri kuwa malezi yanayoelekezwa na dini pekee hayafai kwani hayawezi kulenga vizuri maisha ya kihalisi yalivyo.

Vile vile katika riwaya ya Kezilahabi ya *Rosa Mistika*, (1971), mwandishi ameshughulikia malezi ya watoto. Ameonyesha malezi ya watoto ambao pia wote ni wasichana. Rosa ndiye kifungua-mimba wake na yeye ndiye mhusika mkuu katika riwaya. Maisha yake ya tangu utotoni hadi utu uzimani na hatimaye kifo chake yamemulikwa kwa kirefu. Kama Susan wa *Nguvu ya Sala*, Rosa

analindwa na babake hivi kwamba hawezi kuhusiana na wavulana. Vile vile, kama Susan, alikuwa akipigwa kinyama na babake ilipojulikana kuwa alikuwa na uhusiano na mvulana yeyote. Rosa akiwa katika chuo cha waalimu anakuwa na tabia mbovu sana kwa kuwa na mahusiano yaliyokithiri na wanaume wa kila sampuli. Anaishia hata kuavya mimba. Anapojaribu kuzungumziwa na Padre kuhusu dini na wokovu anakataa kukubaliana na huyo Padre. Mwishowe anaishia kujiua kwa kumeza vipande vya chupa aliyoisaga mwenyewe. Matatizo ya Rosa basi yalitokana na malezi mabaya ya kudhibitiwa kulikokithiri ya babake Zakaria ambaye hakuelewa kuwa watoto wa kike wanafaa kupewa nafasi ya kuhusiana kulikowajibika pamoja na wavulana ili waweze kuwaelewa.

2.5 DINI NA UTAMADUNI

Katika riwaya hii mwandishi ameonyesha kuwa dini haina nguvu juu ya utamaduni wa kijadi. Tunaeleza kuwa karibu na mji wa Richard kulikuwa na mkuyu fulani. Alikuwa ameonywa asiukate na mzee mmoja kwa sababu ni madhabihu, ni mastakimu ya mizimu. Yeye alijibu kuwa imani hizo hazina nafasi katika ulimwengu wa leo na kuwa zimepitwa na wakati. Anasema kuwa yeye amekombolewa na hashikili imani kama hizo. Mzee yule alimwambia aukate kama amekombolewa. Alijaribu kuukata na baada ya kuugonga kwa shoka mara mbili tu, anatokezewa na joka kubwa na kutoroka. (Uk.7-8). Tangu hapo aliugopa mkuyu huo na hakuthubutu kujaribu kuukata tena. Haya yanaonyesha kuwa kulikuwa na nguvu fulani zilizokuwa zikiulinda ule mkuyu ili usikatwe na yeyote asiyependezwa nao. Nguvu hizo hazingeweza kushindwa na nguvu zingine zozote hata za kidini.

Pia wakati Susan, mwanawe Richard, ambaye wakati huo bado alikuwa mkristo, alipopata ugonjwa wa matubwitubwi, nyanyake alikataa apelekwe hospitalini na akamfanyia mambo ya

kishirikina akitumia vigae, ule ugonjwa ulipona kabisa. Ingawa Richard alikuwa mtu wa dini, hakuyapinga haya. Haya yanaonyesha kuwa kwa watu kama Richard, dini zao sio sulubisho kwa kila kitu bali wao bado wanathamini mila na desturi zao. Hizi zinaonekana kufaulu kuliko imani zao katika dini.

Pia Mary, mkewe Richard ambaye pia ni mkristo aliposikia bundi akilia karibu na zizi la ng'ombe, alitupa vigae upande wa hilo zizi na kufuatiza maneno fulani, hili ni tendo la kishirikina na alifanya hivyo ili kujikinga yeye na jamii yake dhidi ya hatari au msiba wowote kutokana na ndege huyo. Katika jamii nyingi za Kiafrika, bundi huchukuliwa kuwa ndege anayeashiria hatari. Jamii hizi basi huwa na njia za kujikinga kutokana na athari za ndege huyo. Hapa tunaona Mary akitupa vigae na kutamka maneno fulani ya kuiondolea mbali hatari inayoashiriwa na ndege huyo.

Kutokana na mifano hii, tunapata kuwa waamini hawa wanachanganya dini pamoja na mambo ya kitamaduni ya kishirikina kuonyesha kuwa hawaithamini dini kwa mioyo yao yote bali wanaona ina upungufu fulani.

Sababu nyingine ya kutenda mambo haya ni mambo yanayohusu akili ya mwanadamu.

Mtaalamu wa mambo ya akili wa Kiswisi, Carl Gustav Jung (1875-1961) alizungumzia uto-ufahamu wa kijumla (pamoja na ule wa kibinafsi) ambao ndio bohari ya tajriba za binadamu na ndio huwa na vikale (yaani taswira za kimsingi ambazo ni bia kwa vile zinajirudia katika tamaduni huru). Utokaji kwa nguvu wa taswira hizi kutoka kwa uto-ufahamu hadi himaya ya ufahamu aliuona ndio msingi wa tajriba ya kidini na mara nyingi ubunifu wa kisanaa. (katika *Encyclopaedia Britannica*, 2003 juzuu la 26: 517).

Katika Brome (1978: 188-189) tunaelezewa kisa kimoja kilichoshuhudiwa na Carl Gustav mwenyewe. Alikuwa ametembelea Jangwa la Sahara, akiwa ndani ya mkahawa aliona watu wengi wakaaji wa jangwani wakivuruta ngamia, nyumbu na punda kwa nguvu. Wanakijiji hawa walitengeneza njia katikati yao ili kiongozi wao apite.

Kiongozi huyo alikuwa amewapa kibarua cha kuchimba mitaro ya maji ya kunyunyizia mimea. Watu wale waliokuwa wamebeba majembe na vikapu walimfuata nyuma yule kiongozi aliyekalia nyumbu wake bila wasiwasi, akiwaongoza wale watu waliokuwa wakicheza kama punguani kama waliokuwa wakienda vitani. Wale watu walianza kuikata ardhi kwa hasira huku wakibeba vikapu vizito vya ardhi na huku wakicheza kwa midundo ya ngoma kadhaa. Kwanzia asubuhi hadi usiku, wale watu waliendelea na tendo lile mpaka walipochoka hivi kwamba kila mmoja wao alijiangukia na kulala kando ya ngamia wao na mwishowe kukawa na ukimya mkali. Yule kiongozi hakuguzwa na zile kelele zote. Baada ya kushuhudia haya, Jung alihitimisha kuwa kuna jambo lililotokana na kundi lile la wanakijiji lililowadhibiti wale watu na kwa hivyo hawangeweza kuyadhibiti matendo yao. Haya pia yalimsaidia kuelezea dhana yake ya uto-ufahamu wa kijumla.

Kwa kuzingatia maelezo haya, tunapata kuwa wanajamii wa riwaya ya *Nguvu ya Sala*, ambao ni wafuasi wa dini ya Kikristo, wanajipata wakitenda mambo ya kimataduni yasiyoafikiana na imani za dini yao. Hii ni kwa sababu ya ule uto-ufahamu wa kijumla, hawana udhabiti mkamilifu wa fikira zao kwa sababu wako katika himaya ya wanajamii wengine ambao hutenda mambo yale ya kishirikina hata bila kufahamu wanafanya vile. Mary anatupa vigae na kufuatisha maneno fulani anapomsikia yule bundi akilia na hili ni tendo la kishirikina ingawa yeye ni Mkristo. Haya ni mambo yaliyo katika uto-ufahamu wake na kwa hivyo hana uwezo wa kujizuia nayo.

2.6 DINI KAMA IMANI ISIYO NA MASHIKO

Mwandishi pia anaibaza dini na hivi kukubaliana na mawazo ya Sigmund Freud (1865-1939) katika kitabu chake, *The Future of an Illusion*, (1961:17) aliyeonelea kuwa watu huzua dini kwa sababu ya woga. Analinganisha wazo la kuwepo kwa miungu au Mungu, na jinsi ambavyo watoto wadogo huwaogopa wazazi wao hasa baba ingawa wao wenyewe wanajua kuwa baba yao angewakinga dhidi ya hatari yoyote. Vivi hivi, binadamu huzipa nguvu fulani za kimaumbile uwezo wa baba, na kuzifanya kuwa miungu. Miungu hawa ndio wanaomwondolea mwanadamu woga unaoletwa na maumbile, kuwapatanisha waja na ukatili wa Jaala au Majaaliwa, hasa kuhusiana na kifo na pia kufidia mateso yote na unyimwaji unaoletwa na maisha yenye ustaarabu. Freud anaangalia dini kama sehemu mojawapo muhimu ya ustaarabu huu.

Tukiangalia ithibati kutoka kwa riwaya yenyewe tunapata kuwa Richard na mkewe Mary hawakuwa na uhakika na mustakabali wao. Jaala ilikuwa imewacheza shere, Richard hakuwa na matumaini tena ya kupata kazi, Mary naye alipata mimba ya mwajiri wake na kutimuliwa. Inakuwa ni kama sadfa wote kuwa katika ule mkutano wa mahubiri kule Uhuru Park. Yule mhubiri kwa maneno aliyoyasema, yaani;

“Ulimwengu umejaa ukatili wa kila aina...”

“Watu wamegeuka makatili.”

“...Matatizo ya ajira, matatizo ya kazi yameongezeka.”

“Mimba zisizotakikana, matokeo ya hila za Lusiferi.

“...Bwana anasema njooni kwangu enyi mnaosumbuka...”

Mnaolemewa na matatizo chungu nzima... Nitawapumzisha!”

“U mgonjwa. Huna kazi. Unajisikia mpungufu. Huna matumaini; una shida kila aina. Mpe Bwana maisha yako leo.”

“Mm...kumbuka leo huenda ikawa siku yako ya mwisho. Huenda ukachukuliwa na Bwana leo ... Mm...kama yule tajiri. Huu ndio wakati wa kutubu. Kifo kinakukodolea macho... Eh ... Ufu huu... mm... Mkubali Bwana.” (uk.158-159)

Anathibitisha kuwa watu wamezizua dini ili wajikinge na matatizo yanayowakumba wanadamu Pia ametumia kigezo cha woga kuwasilii watu wampe Bwana maisha yao, kama Freud anavyosema, wanadamu huogopa kifo sana na wanaweza kufanya lolote ili wajikinge na misiba iletwayo nacho.

Pia kuhusiana na dini kama imani isiyo na mashiko au ya uongo, mwandishi anaonyesha kufeli kwake katika ombi la Richard kuhusiana na mke. Aliomba Mungu kila siku amtunukie mwanamke mzuri wa kuo, (uk.167) lakini badala ya haya, anafanyiwa hila na Mary ambaye tayari keshapata mimba na mwanamume mwingine.

HITIMISHO

Tumeangalia jinsi dini ilivyosawiriwa katika riwaya hii. Mwandishi ameonyesha kwamba katika jamii tunayoishi iliyojaa maovu ya kila aina yakiwemo ufidadi, mauaji, wizi, ukahaba na mengineyo, dini haina nafasi kubwa. Pia ameonyesha kuwa nguvu ya sala au maombi sio jibu la kila tukio na tatizo ulimwenguni.

- Dini haiwezi kuwa suluhisho kwa kila upungufu wa binadamu, na pia haiwezi kusuluhisha matatizo yote ya kimaisha, kwa hivyo ina nafasi duni sana kwa binadamu.
- Mwandishi anapiga tashtiti yale mambo mazuri yote yaliyohusishwa na dini hapo zamani na kuonyesha kama yasiyokuwa na maana katika jamii ya kisasa.
- Mwandishi pia ameonyesha kuwa mafunzo ya dini pekee hayawezi kutumiwa katika kuwalea watoto.
- Mafunzo ya dini pia hayana thamani yoyote wakati mwanadamu anapokumbwa na matatizo ya kimaisha.

Kwa hivyo mwandishi anasisitiza kuwa wanadamu lazima wabebe mizigo ya maisha yao bila kutarajia usaidizi wowote kutoka kwa Mungu au miungu.

SURA YA TATU

3.0 DINI KATIKA RIWAYA YA *WALENISI*

3.1 UTANGULIZI

Katika riwaya ya *Walenisi*, dini imeshughulikiwa kwa namna tofauti. Mwandishi ameonyesha kuwa imani katika dini yoyote ikituniwa vibaya inaweza kuleta madhara na basi haifai kufuatwa. Mwandishi pia anaonyesha kuwa imani ya watu kujazwa tamaa ya maisha mazuri mbinguni ilhali duniani mwamini anasumbuka kwa sababu ya ukosefu wa chakula, maji na mavazi ni potofu. Mbali na haya yote mwandishi ameonyesha kuwa kuna uwezekano wa yale maisha mema yanayoahidiwa mbinguni kuwa mumu humu duniani ikiwa ubepari na unyonyaji utakwisha na ujamaa kuwepo badala yake.

3.2 DINI NA DHULUMA

Kwa mujibu wa Mwita (2003) dini ni kigezo kimoja cha kuwagawa watu duniani katika makundi ili kuyabagua. Wakati Dzombo alipokuwa katika safari ya sayari, alijikuta katika Jabali la Udhalimu bila kutahadharishwa. Huko aliona jinsi wafuasi wa dini walivyogawika na wanavyodhulumiana.

Tunaambiwa:

“... Mkristo mnafiki – kufa!”

“... Utaniona Mwislamu wee – kufa!”

“... Hivi ninakuanza Mprotestanti mkosa adabu wee – kufa!”

“... Hata miguu nitaing’oa mwabudu vinyago Mkatoliki wee – kufa!”

“... Utanisikia leo pagani Mwafrika wee – kufa?”

“... Sitakuwacha Myahudi mlaghai wee – kufa!”

“... Kelb Mwislamu Mwarabu wee – kufa!”

“Niko njiani kukuzika kabisa Mhindi mwizi wee – kufa!”

“Nitakuongezea mrututu mkosa dini mkomunisti wee – kufa!” (uk.30-31)

Mwandishi katika dondoo hili anaonyesha jinsi udhalimu ulivyojaa miongoni mwa wanadini, hakuna anayeithamini dini ya mwenzake na kwa hivyo wanaishia tu kutukanana na kusutana.

Kuna dhuluma kati ya dini tofauti na kati ya madhehebu ya dini.

3.3 DINI KAMA UTAMADUNI WA KIGENI

Mwita (2003), katika mwongozo wake wa *Walenisi*, amenakili mahojiano kati yake na Katama Mkangi, mwandishi wa riwaya hii na alipomuuliza dini ina nafasi gani kati kuleta haki, usawa wa maendeleo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi katika nchi, mwandishi alijibu:

“Dini ni sehemu moja ya utamaduni wa watu. Dini tulizonazo za Wakristo na Waislamu ni tamaduni za Wazungu na Waarabu. Lakini tuiseme kwamba sisi Waafrika hatuna dini kwanza. Katika historia ya kale ni sisi Waafrika ambao tulibuni dini. Sisi ndio tuligundua Mungu kwanza. Wale watu wetu wa zamani wa Misri, ndio waliokuwa waanzilishi wa dini ya kusema kuna Mungu mmoja. Dini ambazo zilikuja hapa, zilikuja na ubepari. Zilikuja na dhuluma. Zimetumiwa kisiasa na kijanja kutufanya sisi wajinga. Sisemi kwamba dini si muhimu. Dini ni muhimu lakini dini hiyo kama vile uchumi iko katika misingi yetu. Dini ina misingi ya kutufundisha kuwa watu bora, kutufundisha nidhamu. Dini zote ni sawa. Mtu asikudanganye.” (Mwongozo uk.50).

Haya ni maneno ya mwandishi mwenyewe. Kulingana naye dini ambazo ziko katika jamii aliyoisawiri ni za kigeni.

Katika riwaya mwandishi ameonyesha jinsi jamii aliyoishughulikia ambayo ni ya Kiafrika iliyoathiriwa na imani za dini hizi za kigeni. Mwandishi aliichukulia dini kama kasumba ambayo anasema kuwa inavutia na kupendeza pia. Aidha ina ishara zinazotatiza na ugonjwa uletwao na miamba hiyo huwa na ishara za namna nyingi zinazokuwa zimejificha. Dzombo alianza kuzikariri ishara hizo:

“Kulikuwa na ile ishara ya kifafa cha kutojijua. Ishara hii ya kasumba humpa mtu hali ya kujitusi bila yeye kujifahamu kuwa anafanya hivyo. Maradhi haya yanatatiza sana kwa kuwa mwenye kuugua huyachukua kuwa ndiyo dawa!

Mtu husema ati hana dini. Matibabu? Kujisweta kwenye dini ya mwingine ili ajiponye. Atapewa oparesheni ya jina jipya, pensilini ya imani mpya, na hata kufanywa mlaji wa nyama na mnywaji wa damu ya binadamu. Thawabu? Kuzoroteka kwa mtu zaidi kwa kifafa, kwa kumpooza ubongo wake hali moyo wake u bado unapiga. Hali hii ya kutojitambua hugeuzwa na ikawa ndiyo ya kawaida kifafa kinapochukuliwa kinamaanisha hali halisi.

Pia, mara myingi kifafa hiki humpoteza fahamu timamu mtu na ukamsikia akisema kuwa ana pesa, hali ukimwangukia mbinu za hizo pesa hazijui ziliko. Yeye kifedha ni kuagizwa nini apande, nini cha kuunda na nini anunue; na kisha kulipwa. Kuagizwa huku hakuishi, naye ndipo azidipo kujinaki kuwa pesa bado ni zake tu!” (uk.26)

Aidha kifafa hiki kinamtia mhasiriwa majeraha ya kuomba kusikoisha ili aweze kujitibu magonjwa aliyo nayo. Hali hii humjaza mgonjwa majipu ya kuombaomba mwili mzima. Hali ya mtu kutokuwa na pesa hujidhihirisha kwa mwili mzima kupachikwa mabendeji ya matibabu ya misaada ambayo humziba mgonjwa macho na kuacha mdomo. Halafu mwenyewe anapewa kijiti na kuongozwa lakini bado anaendelea kukiri kuwa:

“Mimi niko huru. Mimi niko huruu. Mimi niko huruuu.”(uk.26)

Hali hii ya kutojijua husababisha matatizo na humfanya mtu aige ya wengine hivi kwamba anakosa kujithamini yeye pamoja na ukoo wake. Anaona kuwa vyote vyake vikiwemo jina, utamaduni, ustaarabu na chochote chake kingine hakina thamani. La kushangaza ni kuwa yeyote ajitoleaye kumzindua atapewa lakabu kama vile mzushi, mchawi na asiyetosheka. (uk. 27)

Mwandishi pia anasema kuwa kwa vile anayeiga hajui kuchuja, anaishia kuiga yale mabaya pekee, dalili ambayo inajidhihirisha upesi katika lugha ya mtu. Hii humfanya akose hata lugha yake ya kwanza na anatapatapa kujitafutia hewa ya kuweza kujieleza kinaganaga kwa kutumia lugha ya mtawala wake. Anazidi kusema kuwa mwenye maradhi haya lazima awaambukize watoto wake na hivi kuzika mbegu ya kurithisha ishara hii ya kasumba. (uk. 28)

Kutokana na dondoo hizi tunaona kuwa mwandishi ameziona dini zilizokuja na wageni kuwa hazifai kamwe. Anaonelea kuwa dini hizi za aina hii humfanya mtu aonekane aliyepotoka na kumfanya aige yale mabaya ya wenye dini ile. Anaona kuwa hili ni tatizo la kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwani wazazi huwarithisha wanao mbegu za kasumba za wageni. Uigaji huu wa tamaduni za kigeni huwafanya waigaji kuwa kama vinyago tu. Unawafanya watu wakiri mambo yanayowafanya waonekane punguani, kama vile, wakati mtu asiye na hata mbinu za kupata pesa anapokiri kuwa pesa anazo; au wakati mtu amepofuka akili kwa sababu ya kushinda akiombaomba na bado anaendelea kukiri kuwa yu huru.

Hapa mwandishi ameonyesha kuwa utamaduni wote ulioletwa Afrika na wageni hasa dini hauna manufaa yoyote kwa yeyote yule kwa sababu ni potofu na unamfanya mwigaji awe kama

punguani na kumfanya hata apoteze lugha yake ya kwanza jambo linalomkengeusha na kumfanya aonekane mgeti ilhali yu nyumbani kwao.

Pia, wakati Dzombo alikuwa Walenisi, wakizungumza na Mtu-Bint-Fikirini, anayatamka maneno manne ya Kiingereza yaani, *'Yes, I am sorry'*, Mtu-Bint-Fikirini haelewi maana ya maneno haya. Hii inaonyesha kuwa huko Walenisi hakuna athari yoyote ya wageni kwa sababu kiwakilishi kimoja cha athari za kigeni ni lugha mpya na Wawalenisi hawana athari ile ya lugha geni. Wawalenisi wanalichukulia neno *'English'* kuwa *'Iblish'* au Ibilisi. Kutokana na historia ya nchi za Kiafrika, Afrika ilitawaliwa na wakoloni ambao walileta mambo mengi ya kigeni na kuyashindilia kwa Waafrika. Miongoni mwa haya ni dini na lugha. Wakoloni wengi hasa Waingereza waliwashurutisha watawaliwa kuzungumza lugha zao na kuwaambia utamaduni wao ni wa kishenzi na pia kuwa imani zao hazina mashiko. Mwandishi kwa kutumia tukio hili anaendelea kuonyesha kuwa chochote kilicholetwa na wakoloni ni cha kigeni na basi hakifai kutiliwa maanani na Waafrika. Wakoloni na wageni wengine ndio waliokuja na dini nyingi zilizoko Afrika na kuwafanya kutupilia mbali dini za kitamaduni za Kiafrika.

3.4 DINI NA SIASA

Katika riwaya hii mwandishi ameonyesha jinsi dini inavyoingiliana na siasa. Ameonyesha jinsi viongozi wa kisiasa wanavyoitumia kwa manufaa yao binafsi. Kwa kutumia jazanda ya Wachuna na Uchuna, na pia mbinu ya usimulizi kuhusiana na kuasisiwa kwa koo tatu kuu za Wachuna, yaani, Moto, Mchawi na Mabavu, ameonyesha jinsi Wachuna walivyoitumia dini kuwanyamazisha wanyonge. Mchawi ambaye ni mmoja wa waasisi wa Uchuna alitumia ujanja kuzua ukoo wake. Katika riwaya, tunaambiwa kuwa Mchawi alikuwa kichakani akijisaidia alipoyaona majoka mawili, chatu na bafe yakipigana. Kila moja la majoka haya lilikuwa

likijaribu kukwepa mapigo ya lingine. Baada ya muda mfupi, bafe alimpatika meno chatu na kumtapikia sumu yake yote. Chatu aliweza kujinasua na akamuua bafe. Baadaye, yule chatu alijikokota hadi chini ya mti mmoja na kuanza kuchimbua. Alivunja mizizi ya mti huo na kuimeza na pia kutoa magamba na majani ya mti huo na kuyameza. Muda mfupi baadaye, aliondoka pahali pale kwa jinsi iliyodhihirisha kuwa ile sumu ya bafe imemwisha mwilini kabisa. Mchawi naye alichimba ile mizizi, akatoa magamba na kuchuna majani ya ule mti na kwenda nayo nyumbani. Baada ya siku kadha, jirani yake aliumwa na bafe na Mchawi akaenda kumtibu kwa ile mizizi, magamba na majani. Alipokuwa akimtibu alikuwa akiigiza kelele za yale majoka lakini watu walidhani kuwa ni maneno ya kichawi. Yule mtu alipona na ikawa sasa Mchawi pekee ndiye angeweza kumtibu yeyote aliyeumwa na nyoka. Kwa wale ambao walikufa, ilisemekana kuwa ni bahati mbaya. Mwishowe Mchawi aliletewa wagonjwa wa kila sampuli kuwatibu. Kazi ilipozidi akawaambia wanakijiji kuwa ilimbidi naye pia aende kondeni ili ajilisha lakini wao wakasema kuwa watamlisha. Kwa njia hii aliweza kujilimbikizia mali nyingi na akawa na uwezo mwingi sana kiuchumi na hakuwapa wengine siri ya nguvu zake isipokuwa kuwarithisha watoto wake wa kiume na kuwalisha kiapo wasiitoe siri hiyo kwa mtu mwingine yeyote. Hivi ndivyo ukoo wa Uchawi ulivyozuka. Kama tulivyoona, ilitokea kisadfa tu Mchawi kushuhudia vita kati ya majoka yale na kwa kutumia hila na ujanja mwingi aliweza kujitajirisha, yeye na ukoo wake wote. Tunaambiwa kuwa wachochole hujazwa na wanasiasa kasumba kuwa watakuwa sawa na kuishi maisha bora watakapofika juu Mbinguni. Wanafundishwa kuwa na subira na kutowaonea wivu wenzao kwani kufanya hivyo ni dhambi. Wanasisitiziwa pia kuwa wasijichukulie kama raia wa duniani mnamomithilishwa na Jehanamu, bali ni raia wa Ufalme wa Mbinguni ambako taabu zao za kimaisha wanaambiwa zitakoma. Haya yalikuwa majibu ya Dzombo kwa Wawalenisi waliotaka kujua kwa nini hakuna usawa duniani. Dzombo pia anakiri kuwa dini zote duniani zinawatia watu kasumba ya aina hii. Hizi pia zinasisitiza kuwa ingawa

Mungu alituumba sawa, usawa wenyewe utapatikana tu baada ya kufa, yaani huko Mbinguni, kwa Mwenyezi Mungu. Kwa kutumia kasumba hii waliweza kuwapumbaza raia na kuwafanya wasipigane haki zao bali wakae tu na kungojea maisha mema yenye fanaka huko Mbinguni

Baada ya kuzuka kwa koo tatu za Wachuna: Moto, Mchawi na Mabavu, hawa walisitiza kuwa walizaliwa na akili nyingi kuwazidi wengine wanaowatawala na haya ni mapenzi ya Mungu mwenyewe. Pia walisema kuwa binadamu hawakuumbwa sawa, wako tofauti kama vidole na bila shaka hayo ndiyo mapendekezo ya Mola Mwenyewe, wao hawawezi kuyapinga. (uk. 169)

Wachuna pia walisema kuwa sio lazima mtu ale na shibe bali haya yanategemea bahati ya Mungu tu na hata wakanukuu kifungu cha Bibilia kisemacho kuwa “binadamu hataishi kwa mkate peke yake.”

Pia tunaambiwa kuwa akina yakhe wakati mmoja walikosa maji kwa sababu yalikuwa yamechukuliwa yote na matajiri na kuyaoshea hata majibwa na mapaka yao. Bunge kwa kuwaonea huruma hao wasiobahatika likawasilisha hoja ya kuwaamrisha kuwa baada ya kuyaoshea majibwa na mapaka, hayo maji yatiwe mapipani na wapelekewe waduni. Kitendo hiki kilisifiwa sana na magazeti na wakuu wa dini walichokiita, “cha ukarimu mkuu.” (uk. 175). Tukio hili linakusudiwa kuonyesha jinsi asasi ya dini ilivyotumiwa na inavyotumiwa na serikali dhalimu kuhlalisha udhalimu na ukatili. (Wamitila 2003b:51).

Pia tunaelezwa kuwa zile koo tatu za Wachuna zilionesha mafiga matatu nyoyoni na akilini mwa waja, yaani Figa la Uoga, la Ulafi na la Ujinga. Lile la Uoga likazua bunduki, mabomu na vikosi vya askari kama vile “Hebu Fanya Fujo Uone (HFFU),” ili kuwaogofya watu zaidi wasiweze

kupigania haki zao na kujikomboa. Umma ukatiwa hofu zaidi kwa mabavu kutoa sheria na sheria ikazua magereza. Uchawi nao ukazua dini, nayo dini ikavumbua Jehanamu na Peponi ili kushindilia zaidi Figa la Uoga kwa kuwapumbaza na tamaa za baadaye. Wachuna wenyewe hawakuwa na tamaa hii bali ilitiwa tu akilini mwa wachochole, jambo lililowafanya hawa wawe tu kama magofu. Figa la Ulafi lilisifiwa na msemo wa Wachuna kuwa. “Kila mtu peke yake, na Mungu awe wetu sote”(uk. 189). Figa hili liliwafanya wahodhi nyenzo zote za uzalishaji mali, biashara zote zikawa ni zao na ndio wakazua msemo ule ili kuutetea ubinafsi ule wao.

Pia, wanyonge katika enzi za Wachuna walipewa elimu ya kidundu isiyo na hekima yoyote; ya kuwafumba macho tu. Wanyonge waliendelea kuteseka kwa ukosefu wa lishe na mahali pa kuishi ilhali Wachuna waliendelea kunufaika na maendeleo ya kisayansi na kiufundi. Wanyonge waliambiwa: “Subira. Baba yenu aliye Mbinguni atawatimizia yote huko Akhera, dini iliwaliwaza na wakaliwazika.” (uk.192). Haya pia ni matumizi mabaya ya dini na viongozi wa kisiasa.

Wachuna walikuwa wakiwatupia wanyonge vijipande vya nyama na kwa uhaba wa walivyotupiwa walipapurana kukatana meno na kutiana makucha wakipigania hayo makombo. Wachuna waliwacheka na kujifanya hawakuelewa chanzo cha tabia ya ushenzi wa wanyonge ingawa walitambua kuwa walitawalika kwa urahisi baada ya kufuzu kwao katika ushenzi huo na:

“Isitoshe dini nayo wakapewa bure – jambo ambalo liliwapatiliza kwa kuwagongomeza zaidi ujingani: Wachuna wakawa sasa wakiweza kulala raha mustarehe, hali wanyonge wakawa wakikeshwa usiku kucha wakiomba Mungu! Ulafi ukawa umewadidimiza ndani ya Figa la Ujinga, na likawa silaha kubwa mikononi mwa Wachuna. Walitambua hivyo ndipo walivyokuja na msemo uliosema: ‘Usimwamshe aliyelala ama utalala wewe.’” (uk. 190-191).

Wachuna walitumia dini kama chombo cha kuwadidimiza zaidi katika ujinga ili wazidi kuwatawala. Wao wenyewe walilala vizuri huku wakiwafanya wanyonge kulala wakiomba Mungu ili nao pia wapate maisha yenye faraja. Wachuna walivicheka vitendo hivi vya wanyonge na kuwachukulia kama waliolala, hawangetaka kuwazindua kwani walijua kuwa kuzinduka kwa wanyonge ndiko kungekuwa maangamizo yao.

Wakati mmoja Dzombo akizungumza na Mtu-Bint-Fikirini, anaelezwa jinsi mateso ya wanyonge chini ya mfumo wa kidhalimu wa Wachuna yalivyoundwa mkono na asasi ya dini. Anaambiwa:

“La kusikitisha ni kwamba kulikuwa na chungu nzima ya wataalamu bandia wa elimu-jamii na viongozi wengi wa dini waliounga mkono upuuzi huo.” (uk.103)

Vivi hivyo ndivyo ilivyokuwa katika nchi ya Dzombo na ndiyo sababu anasema:

“Jehanamu, tunaamini kama wao wataalamu wenu bandia na viongozi wenu wa dini walivyofundisha.” (uk.103)

Jamii ya Wachuna iliyotangulia kujengwa kwa jamii yenye usawa ya Walenisi ilikuwa na wataalamu bandia na viongozi wa dini wanafiki. Mtu-Bint-Fikirini alidokeza kuwa Wachuna waliwalinganisha binadamu na siafu, nyuki na mchwa. Kwa kusema haya, hawa walikuwa wakitaka kusesitiza kuwa tofauti za kijamii, asili zao ziko katika sheria za kimaumbile.

(uk. 102-103).

Ingawa jambo kama hili halifai kamwe na lingefaa kukataliwa kinywa kipana, wataalamu wanaoitwa bandia na viongozi wa dini walikubaliana nalo kabisa; kulinganisha akili za binadamu na za wadudu na kwa kufanya hivi kukiri kuwa maarifa ya binadamu hayawezi kuzidi silika jinsi yale ya wadudu, wanyama, samaki na wengineo yalivyo.

Mwandishi ameonyesha mchango uliopo wa dini, hasa matumizi yake mabaya, katika kuwadhalilisha binadamu kutikia hata kiwango cha kuwamatilisha na wadudu. Katika historia ya ukoloni katika Bara la Afrika, kuja kwa wakoloni na utawala wao wa kidhalimu kulienda sambamba na matumizi ya dini ya Kikristo. Dini hii inaendelea kutumiwa kwa malengo sawa na uongozi wa mataifa hayo huru ili kuhafalisha udhalimu na unyonyaji (Wamitila 2003b:50)

Pia kuna ile hali ya kuweka maisha ya wanyonge katika imani ya majaliwa au jaala. Hii ni imani kuwa maisha ya binadamu yanatawaliwa na nguvu zenye uwezo kumshinda na nguvu hizi mara nyingi huwa za Kiumbe aliye na uwezo zaidi ya mwanadamu na hivi basi, mwanadamu hana uwezo wa kuzikwepa.

Kwa mujibu wa riwaya hii, imani kama hii yaweza kumfanya mnyonge asijibidiishe kwa lolote lile ili kujikomboa. Tunaambiwa:

“Hivi inamaanisha kuwa aliyenacho anajitoa kwenye lawama kwa kukataa uhusiano uliopo baina yake na yule asiyenacho; na kwamba ni kwa ukarimu wa aliyenacho ndio utakaomfanya asiyenacho kuishi? Upuzii ... upuzi mtupu!” Mama Mtu-Maanani akawa anamsimulia mumewe.

“Pia na zaidi, inamaanisha kuwa huko Jehanamu wanaamini kuwa Mungu wao, Ibilisi, ndiye mpaji wa yote mema na mabaya. Ukipata mema umshukuru yeye; ukipata mabaya pia useme ‘majaliwa’, Mzee Mtu-Mwenzio akawa anaendeleza mazungumzo.

(Uk.124-125).

Kutokana na dondoo hii, mwandishi anawahimiza wanyonge wajitahidi ili kujinasua kutoka pingu za maisha yao; haya ni hasaa kwa kumtumia mhusika Mama Mtu-Maanani kuyarejelea

maoni ya walio nayo kuwa ni upuzi mtupu. Mwandishi anaendelea tu kushambulia matumizi mabaya ya dini katika utawala wa Wachuna na pia huko nchini kwa kina Dzombo. Hawa waliitumia dini kuwapumbaza wanyonge wasitamani hali na maisha ya walio navyo kwa kuwa vyao vinawasubiri baada ya kufa kama tulivyoona hapo juu.

Mifano hii yote inatodokezea jinsi wanasiasa na viongozi wenye mali wanavyoitumia dini kuwanyamazisha akina yakhe wasitetee haki zao kwa kuwatia kasumba kuwa mali yao iko mbinguni kwa hivyo wavumilie mateso yao kwani ni ya hapa duniani tu. Pia viongozi wa dini wanaviunga mkono vitendo visivyo vya haki vya wakuu kama katika kile kisa cha maji yaliyoyaoshea majibwa na mapaka kupewa wachochole, na pia kukubali kuwa binadamu ni sawa na jamii za wadudu kama vile siafu, nyuki na mchwa.

Hapa pia mwandishi anakubaliana na Napoleone Bonaparte, aliyekuwa mtawala wa Milki ya Ufaransa, aliyewahi kusema kuwa 'Dini wajibu wake mkuu ni kuzuia maskini wasiwauwe matajiri'. (Andala 2003: 28-29).

Mwandishi ametumia kinaya na tashtiti kuonyesha kuwa matendo ya wanasiasa hao ni ya kinafiki na ya kibinafsi.

3.5 RIWAYA KAMA KAZI YA KIMBAZI

Wamitila (1998: 89) anasema kuwa riwaya ya Walenisi inaweza kumithilishwa na kile kisa katika Bibilia cha Mwana Mpotevu (Luka 15: 11-32). Anasema tofauti ndogo iliyopo ni kuwa katika usimulizi wa Bibilia, mwana yule alitaka kuondoka mwenyewe. Hakuna kani inayoelekezwa kwake inayomsukuma na kumfanya atoroke kwao. Mambo yanapomwendea

mraba huko nje, anarudi kwao baada ya kupitia uzazi mpya wa kiroho na kiakili. Katika riwaya ya *Walenisi*, Dzombo anatoroshwa nchi yake na ukatili na udikteta wa viongozi – ambao ndio kani inayomsukuma. Baadaye shujaa huyo anarudi nchini mwake baada ya kuzaliwa upya kiakili jambo linaloonyeshwa kifumbo na kifo-tarajiwa chake. Kwa hivyo hii ni kama kupindua mambo juu chini kwa mbazi ya Kibibilia.

Kama tunavyoona katika maoni haya ya Wamitila, Dzombo na masaibu yake wanaweza kumithilishwa na yule mwana mpotevu aliyetumika katika ile mbazi. Yule mwana alitaka tu agawiwe mali yake na akatoroka nyumbani na kuenda alikoyafuja kwa nyendo zote mbovu, baadaye anapoteseka na hata kukosa chakula na malazi, anajisaka na kujitambua na kukiri na kuyatubu makosa yake na anaporudi nyumbani anapokelewa kwa shangwe na kufanyiwa karamu isiyo kifani. (Luka 15:11-32)

Kwa upande wake, Dzombo hakujitorosha nyumbani, alijaribu kutetea haki zake na wanyonge wenzake na kwa kufanya hivi akawa ni kama anataka kuwamwagia unga viongozi dhalimu, ndiposa akahukumiwa kifo kwa sayari. Anapotoroshwa hawi na chochote cha kuita chake lakini anapofika huko Walenisi, mambo yanamtengenea na anapata hata kuwa Wawalenisi walikuwa wakimgojea kwa muda mrefu. Ilikuwa imetabiriwa tangu jadi kuwa Dzombo angefika huko Walenisi. Wawalenisi walidhania kuwa Mwenyezi Mungu aliishi duniani walikokuita mbinguni na kwa hivyo walifikiri kuwa yeyote atokaye duniani ametumwa na Mungu (Mulungu) na hata walijichukulia kuwa viumbe hafifu wakijilinganisha na wale wa Mbinguni-duniani, alikotoka Dzombo. Huko alitunukiwa yote yaliyo mema na kuchukuliwa kama mungu wa aina fulani. Huko pia anaenda katika *Safari ya Utu*, ambayo ni ya kujisaka, kujitambua, kukiri na kutubu makosa yake. Pia anaenda Mapenzoni, mahali pa utawala pa Walenisi penye mapenzi na usawa wa hali

ya juu. Haya yote yanamfanya azaliwe upya, kiakili na kiroho; anagundua utu wake na baada ya kumuoa Mtu-Bint-Fikirini anaamua kurudi kwao Jehanamu (Duniani) ili akahubiri ule usawa na mapenzi ya kiutu.

Tunaweza kuhitimisha kuwa sababu ya mwandishi kusawiri hadithi yake kama ile mbazi ya Kibibilia ikiwa imepinduliwa juu chini, ni kuonyesha kuwa sio yote yanayohusiana na dini huwa ni mabaya, kuna yale ambayo huwa na mafunzo mema kwa jamii yoyote ile, hasa kama yanahusu kujisaka na kujielewa vyema zaidi.

3.6 WIGOBEZI KATIKA RIWAYA YA *WALENISI*

Wigobezi ni dhana inayoelezea mbinu ya kifasihi ambapo kazi fulani inaiiga nyingine ingawa kuiga huku huwa ni kwa kinyume au kwa njia ya kubeza kazi au mandishi asilia (Wamitila 2003:124). Katika riwaya hii, tunaambiwa kuwa Dzombo anapokwenda Mapenzoni akiwa kule Walenisi, kuna amri kumi zinazosomwa kuhusu msimamo na itikadi ya Wawalenisi. Amri hizi ni:

- (1) “Si dhambi kuwa ulimi wa mabubu wa uoga.”
- (2) “Si dhambi kuwa macho ya vipofu wa ufahamu.”
- (3) “Si dhambi kuwa masikio ya viziwi wa ukweli.”
- (4) “Si dhambi kuwatetea wanaonyanyaswa.”
- (5) “Si dhambi kulia na wanyonge.”
- (6) “Si dhambi kuwakinga waliotiwa mapingu na minyoyoro.”
- (7) “Si dhambi kujitambulisha na maskini hohehahe.”
- (8) “Si dhambi kukomesha vilio vya wateswao magerezani na makorokoroni.”
- (9) “Si dhambi... tena si dhambi: kuusaliti “Uchuna!!!”
- (10) “Si dhambi kupigania haki na usawa wa kila binadamu!!!! Si dhambi!”

(uk. 207-209)

Amri hizi ni wigobezi wa Amri Kumi zinazopatikana katika Biblia katika kitabu cha Kutoka 20:

2-17. Hizi ni:

- (1) Mimi ndiye Mungu wenu, niliyewatoa utumwani Misri, msiwe na miungu wengine badala yangu.
- (2) Msijiundie vinyago au mfano wa chochote kile kilicho juu mbinguni au chini duniani au kilicho majini chini ya ardhi, msiviabudu au kuvitumikia, mimi Bwana Mungu wenu ni mwenye wivu nazifikisha dhambi za mababa kwa wana wao hadi kizazi cha tatu na nne cha wanaonichukia na kuwaonea huruma maelfu wanaonipenda na kutii amri zangu.
- (3) Usilichukulie jina la Bwana Mungu wako kimzaha kwani Mungu hatamtoa lawamani afanyaye hivi.
- (4) Kumbuka siku ya Sabato uiweke ikiwa takatifu, fanya kazi zako zote kwa siku sita, lakini siku ya saba ndiyo Sabato, usifanye kazi yoyote, wewe mwenyewe wala mwanao wa kiume au wa kike au kitwana au kijakazi wako, au ng'ombe wako, au mgeni aliye kwako. Siku sita Bwana aliumba mbingu na ardhi na bahari na vyote vilivyomo na akapumzika siku ya saba na hivyo akaibariki na kuitakasa.
- (5) Mtii baba yako na mama yako ili siku zako za kuishi katika nchi uliyopewa na Bwana Mungu wako ziwe na fanaka.
- (6) Usiuwe
- (7) Usizini
- (8) Usiibe
- (9) Usitoe ushuhuda wa uwongo kuhusu jirani wako.
- (10) Usitamani nyumba ya jirani yako au mke wake au kitwana wake au kijakazi wake wala maksai wake, wala punda wake au chochote kilicho chake.

Dini imetumiwa kuwanyanyasa walio wanyonge. Tukizingatia hasa amri ile ya kumi inayowakataza watu kutamani chochote cha jirani, tunapata kuwa kulingana na mwandishi hiyo amri ilitumiwa na wakwasi kuwanyamazisha wachochole. Tunaambiwa:

“Kwa kuamini nao pia watakuwa sawa na kuishi maisha bora watakapofika juu Mbinguni.

Kwa hivyo wanafundishwa kuwa na subira na kutowaonea wivu wenzao. Wanaambiwa kufanya hivyo ni dhambi.” (uk. 145).

Hapa kama tulivyodokeza hapo juu amri ile inawanyamazisha wachochole kwa kuwaambia kuwa kutamani na kuonea wivu vya wengine ni dhambi.

Tunaweza basi kuhitimisha kuwa mwandishi ameiga zile Amri Kumi za Bibilia kwa namna hii kuonyesha kuwa zile hazimtetei mnyonge kwa lolote lile, jambo ambalo yeye mwenyewe amelisisitiza katika kazi yake na analoona kuwa ndio muhimu zaidi. Kulingana naye, dini yoyote ile lazima ipigie domo unyanyasaji wa wanyonge wala sio kuuunga mkono alivyoonyesha. Zile Amri Kumi za Wawalenisi ni kama kielelezo cha mwandishi cha jinsi amri za dini zinavyofaa kuwa hasa katika ulimwengu wa sasa ambao umejaa dhuluma na mateso katika nyanja zote za maisha.

3.7 RIWAYA YA WALENISI, UMAKSI NA DINI

Kwa kiasi kikubwa mwandishi wa riwaya hii amechukua mtazamo wa kimaksi. Ameonyesha jinsi jamii mpya inavyoweza kujengwa na kudumishwa katika misingi ya ujamaa. Mwandishi ameonyesha jinsi ubidhaaishaji ulivyotumika kudhalilisha wanyonge. Huu ni mfumo wa kuzalisha kitu sio kwa nia ya kukitumia bali kubadilishwa katika mfumo wa kibepari wa soko. Bidhaa hizo zinathaminiwa kutokana na bei zinazoweza kuvuta wala sio kwa kazi yake. Sifa hii ya ubidhaaishaji inaishia kuwahuu binadamu wasiothaminiwa kama binadamu ila kutokana na

uwezo wao wa kuzalisha mali (Wamitila 2003a:184-185). Tabaka tawala ndilo linalosisitiza ukuzaji wa bidhaa za aina hiyo na vyombo kandamizi na vile vya Ki-itikadi vya Dola ndivyo vinavyotumiwa kuhakikisha haya yametendeka. Tukiangalia idhibati kutoka kwenye riwaya, tunaambiwa kuwa Dzombo alikuza mahindi shambani mwake lakini yalipoanza kutoa pungu, matrekta yalikuja na kuyafyeka bila hata kumuarifu. Anapolalamikia haya anaambiwa:

“Ungekuwa umepanda kahawa, kakao, pareto – ama hata maua ya waridi au katani, haingekuwa neno, lakini sio mahindi!” (uk.17)

Naye Dzombo alipouliza angekula nini baada ya kupanda mimea hiyo isiyolika alijibiwa:

“Nchi ingefaidika kwa kupata fedha za kigeni.”

Hata baada ya kupanda mimea ile aliyoambiwa, bado anaambulia patupu na ndiposa katika kujaribu kutetea haki zake, anazikanyaga nyayo za watawala na kuishia kuhukumiwa kifo kwa sayari. Vyombo Kandamizi vya Dola kama vile vikosi vya askari kama, “Hebu Fanya Fujo Uone” na vitisho vya magereza, vilitumiwa kuwanyamazisha watu. Vitisho hivyo vilishindiliwa nguvu kwa kuzuliwa kwa dini iliyovumbua Peponi na Jehanamu ili kushindilia zaidi uoga kwa kuwapumbaza wachochole na tamaa za baadaye.

Marx mwenyewe kuhusiana na dini alisema:

“Dini ni ishara ya kiumbe aliyekandamizwa, moyo wa ulimwengu usiyo na moyo, jinsi ilivyo roho ya hali isiyo na roho. Ni muhadarati wa wengi.”

(Gehman 1993:37) (Tafsiri yetu).

Kulingana na Marx, dini hutumiwa na jamii za kibepari kuwalinda wenye mashamba kutoka kwa mafalahi walio maskini walio chini ya uthibiti wao. Amri zile kumi ni hila ya kuwazuia wafanyi kazi wasipindue mambo. Ubepari umezua dola na sheria zake, dini na majukumu ya kimbeko, ili

kuwatumia wafanyikazi maskini walio wengi ili mabepari waendeleo kufurahia utumishi wa watumwa. Ndiyo maana Marx akahitimisha kuhusu dini kuwa ni “muhadarati wa walio wengi.” Dini huwapumbaza na kuwalaza watu kwa kutumia imani yake katika Mungu na matumaini ya hapo baadaye ya Mbinguni.

Kulingana na wanaoshikilia mtazamo huu wa Umaksi, dini ni lazima ipigwe marufuku ili watu waweze kuishi kiutu. Lenin, mmojawapo wa hawa alisema kuwa maovu ya dini yamo katika zile athari zake za kulevya zinazowatoa wanadamu kutoka kwa dunia halisi. Dini, kama pombe inamlevya mtu hivi kwamba mlevi hayumo katika uhalisi. Badala ya kuzinduka na kuwapinga wanaowakandamiza, wanatabaka la wafanyakazi wanaota tu kuhusu mbingu ijayo yenye majumba makubwa na barabara za dhahabu. Kwa hivyo wale wafanyikazi wanaokandamizwa wananyimwa maisha mema humu duniani kwa sababu wanaotea na kutumainia maisha mema huko mbinguni. (Gehman 1993: 37-38). Vyombo vya Ki-itikadi vya Dola pia vilitumiwa kuwanyamazisha maskini. Hivi ni kama vile asasi za sheria, siasa, elimu na kadhalika. Mojawapo ya itikadi yao ni kuwa kugawika kwa jamii katika matabaka ni maumbile, hivyo basi ni jambo lisilozuilika.

Katika riwaya yenyewe tunaambiwa:

“Wakiendelea kujitofautisha, Wachuna wakasisitiza kwamba, kuishi kwao vyema kwa kweli haikuwa ni kwa kupenda kwao lakini, ni kwa sababu ya kuzaliwa na akili za kuwazidi wenzao. ‘Haki ya Mungu,’ waliapa, ‘Si kwa kupenda kwetu, ni kwa kudra zake Mungu Mwenyewe – na makusudi yake hayabainiki. ‘Lakini,’ waliendelea kwa sauti ya asiyefahamu ahisi dalili za huruma, ‘inaonyesha wazi kwamba binadamu hawakuumbwa

sawa. Tuko tofauti kama vidole. Bila shaka, haya ndiyo mapendekezo ya Mola Mwenyewe, sisi tu akina nani kuyapinga?” (uk. 169)

Katika dondoo hii, asasi ya siasa ndiyo imetumiwa kutetea hoja kuwa jamii kutotoshana hasa kiuchumi ni maumbile na ni mapenzi ya Muumba Mwenyewe na hivyo hakuna binadamu awezaye kuyabadili haya. ‘Wasiobahatika’ wanafaa kutosheka tu kwani ndio maumbile.

Nyaundi, N. (2003:122) anasema:

“Dini huelezea ni kwa nini matajiri wanafaa kuendelea kuwa matajiri na huwaliwaza maskini kwa kuwa katika hali ile. Ukristo huhusisha utajiri na baraka za Mungu na umaskini hutazamwa kama kutopendezwa kwa Mungu. Hili hujenbga wazo kuwa kutotoshana kiuchumi ni mapenzi ya Mungu. Wanasosholojia hudai ukristo unaposema kuwa “Heri ni nyinyi maskini kwani Ufalme wa Mbinguni ni wenu,” (Luka:6:20) basi ni kuwezesha dini kuzuia maskini kuwadhuru matajiri, kwa vile wengine huenda waliyapata mali yao kwa kuwanyonya maskini au kwa njia zisizo halali. Dini ina nguvu za kuvunja au kujenga uchumi.”(Tafsiri yetu)

Pia Weber (katika Nyaundi, 2003:123) anasema kuwa kuna makundi mawili ya watu kategoria mbili, yaani waliobahatika na wasiobahatika. Anasema kuwa dini hutoa halalisho ni kwa nini waliobahatika na wenye uwezo waendeleo kushikilia uwezo ule na kubahatika. Pia inaelezea hadhi katika jamii ya wasiobahatika na inawazuia kujaribu kubadilisha mpangilio uliopo wa kijamii.

Sababu tulizotoa hapo juu ndizo zilizowafanya Marx na Engels na wafuasi wao kupinga dini kwa kinywa kipana. Walionelea kuwa dini ilikuwa pingamizi kwa maendeleo. Mwandishi wa riwaya ya *Walenisi* anaelekea kukubaliana na maoni haya ya Marx asilimia mia moja katika kazi yake

hii. Yeye pia angependekezwa watu kutojali dini na kupigania haki na usawa hadi pale ambapo wangepigania kiwango cha hali ya juu zaidi kilichofikiwa na ulimwengu alioumba wa kinjozi wa Walenisi. Kama Andala (2003:30) anavyosema, “Wawalenisi hawakujali dini sana bali walianza mfumo wa usawa na utu ambapo kila mtu alimpenda na kumheshimu mwenzake kama ndugu.”

Kwa hivyo, kulingana na mwandishi, kilicho muhimu sio imani katika dini bali ni usawa na utu.

3.8 DINI KAMA SULUHISHO

Ingawa mwandishi wa riwaya ya *Walenisi* ameonyesha kwa kiasi kikubwa jinsi dini ilivyotumiwa kwa manufaa ya wachache, huku walio wengi wakiendelea kudidimizwa nayo katika lindi la umaskini, ameonyesha pia kuwa ikitumiwa vyema au ikitazamwa kiyakinifu, inaweza kuleta mabadiliko mema katika jamii. Wakati Dzombo alipotembelea Kamati ya Kiwanda cha Trimi aliona usawa wa hali ya juu sana. Hivyo basi aliamua kuwatobolea Wawalenisi hali mbaya iliyo kwao Duniani. Anaeleza jinsi ambavyo kunasemekana kuwa duniani kuna viongozi ambao, bila wao hakuna lolote linaloweza kutendeka na kuwa imani hiyo imekuwa kama dini kwao. Pia anaeleza kuwa duniani kuna dini nyingi na zote zinafundisha kuwa kuna wenye akili wanaostahili maisha bora kuliko wengine. Wawalenisi wanaposikia haya wanashtuka sana na kumwambia kuwa wao walishagundua siri moja, ambayo ni:

“Yakuwa Mungu ni mapenzi na kwa hivyo basi, katu hawezi kuwabagua wanawe: huyu amfanye tajiri na huyu maskini; huyu amlishe na amvishe akiwa angali hai, na huyu amtaabishe katika uhai wake na amlishe na kumvisha baada ya kufa kwake? Huyu amfanye mtumwa, na huyu bwana wake? ... Haiwezekani. Haiwezekani kwa kuwa Mungu sivyo alivyo... Mungu ni mapenzi. Na mapenzi ni usawa; na usawa ni zao la ushirikiano; na ushirika, ni mbinu zisizoisha za kuupisha ubinadamu wetu. Kwa kutumia kwa pamoja, vipawa vyetu tofauti.”

(uk.146).

Wawalenisi waliendelea kusema:

“... Lakini ni baada ya watu kufahamu kwamba Mungu atutaka kila mmoja wetu - tukiwa papa hapa kabla hatujafa, kuishi kwa usawa, fanaka na raha mstarehe -” na pia.

“...ndio tukauita Ulimwengu huu wetu WALENISI ili kusisitiza ukweli usemao kwamba, ‘maslahi yangu na ya mwenzangu hayabandukani.’ Sasa tumethibitisha kuwa hivi ndivyo Mungu atakavyo tukiwa papa hapa.” (uk.146).

Dzombo anatafakari na kuyakariri maneno ya Sala ya Bwana, yaani:

“Baba yetu uliye Mbinguni,
Jina lako litukuzwe. Ufalme wako
Nauje. Mapenzi yako yatendeke
Hapa Duniani kama yatendekavyo
Huko Mbinguni...” (uk.147)

Hapa ndipo naye pia anapogundua kuwa mapenzi ya Mungu yanatakikana kutendeka papa hapa Duniani. Pia akakumbuka kusoma kuwa kwa Mungu Mbinguni wote watakuwa sawa na pia hakuna machozi, kuumwa au kufa njaa. Lakini kulingana na Sala ya Bwana, haya yote yanafaa yatendeke papa hapa Duniani. Ndiposa akajiuliza:

“Imekuwaje basi nikagomezwa na kasumba ati mpaka Mbinguni? ... Duniani kuwe sawa na Mbinguni?” (Uk. 147)

Dzombo akaona kuwa Wawalenisi walifahamu hayo na wakawatimua watesi wao Wachuna na na ndiposa wakaweza kuubadili ulimwengu wao kuwa kama Peponi Mbinguni.

Wawalenisi pia walimwambia:

“Wachuna, katika ulaghai na unafiki wao walimgawa Mungu vipande viwili – kwa kusema kile kipande kilichokuwa hai kilikuwa ndicho chao, na kile kilichokuwa kimekufa kikawa ndicho cha watwana na vijakazi wao.” (uk. 148)

Wawalenisi pia walimweleza kuwa:

“Haya basi, na hivyo ndivyo mwisho wa Wachuna ulivyosibu – yaani baada ya umma kuzinduka juu ya ukweli usemao kuwa Mungu wa kweli ni yule anayekufaa kabla hujafa. Yaani, kipande hiki cha uhai ambacho Wachuna walikuwa wameking’amua kutoka kitambo na kwa hivyo, wakawa wameking’ang’ania na kuifanya kuwa siri yao kubwa.” (uk. 149)

Kutokana na dondoo hizi zote, ni dhahiri kuwa mwandishi anataka watu wafunue macho na kudadisi mambo ya dini kwa undani zaidi, wasiyaamini yote wanayoambiwa na viongozi dhalimu wa kisiasa na kidini. Ameonyesha kuwa dini inaweza kuwa na manufaa yoyote pale ambapo inawasaidia wote kwa usawa bila kumpendelea huyu na kumdhalilisha yule. Dini ikieleweka sahihi na kutumiwa vizuri inaweza kuwa na manufaa na kuleta usawa kiasi cha kuufanya ulimwengu uonekane kama Peponi. Haya anayashindilia kwa kutumia ulimwengu wa kinjozi wa Walenisi ambapo pana usawa na ushirikiano unaopafanya paonekane na Dzombo aliyetoka Duniani kwenye ubinafsi na dhuluma, kama Peponi.

Pindi tu Wawalenisi walipogundua ukweli kuhusiana na maswala ya Mungu na dini, waliweza kuwapiga vita Wachuna wanafiki na kuleta siasa za ujamaa badala ya zile za ubepari.

Pia, wakati Dzombo na wenzake walipokuwa kwenye Safari ya Utu kule Walenisi, akiwa ndani ya Trimi alijionea jinsi ulimwengu wa Walenisi ulivyopendeza na kila sehemu ilitumika kwa mradi fulani wa kuinufaisha jamii yake kwa jumla. Anafikiria:

“Hii ni lazima iwe ni kazi ya Mungu.” (uk. 52)

Mwenzake Mtu-Bint Fikirini anazikana fikira hizo za Dzombo na kusema kuwa ni kwa juhudi zao. Pia mtu-wazo anamwambia kuwa ngano zao:

“Zinatufunza kwamba hapo zamani, kulikuwa na watu waliokuwa wakikaa vile umekaa nao hawakuwa wakiacha kumsifu Mungu kwa ziada zote walizojipatia kutokana na juhudi za wengine.” (uk. 52)

Dzombo anaona kuwa haya ni sawa na yaliyokuwa yakitendeka Duniani.

Mwandishi anataka kusisitiza kuwa maendeleo yoyote yale hayaji wakati watu wamekaa tu chini na kumwomba na kumshukuru Mungu, bali huletwa na juhudi za kila mtu kwa ushirikiano wenye usawa kama ilivyokuwa kule Walenisi. Yeye anaona kuwa kuombaomba huku hakuna manufaa ila humtia mwombaji majipu ya kuombaomba mwili mzima. (uk.27)

3.9 DINI KAMA IMANI TATANISHI

Katika riwaya hii, mwandishi amesawiri imani katika dini kama iliyo na utata mwingi kiasi cha kutoeleweka. Dzombo anaporushwa kwa sayari na kutua katika nchi anayokuja kuelewa baadaye ni Walenisi, anadhani kuwa amefika Mbinguni kwa Mwenyezi Mungu, basi anategemea kupata ‘Mana’ na ‘Maji ya Kumaliza Kiu Milele,’ lakini anapoulizia haya anaambiwa:

“Unahitaji Mana na Maji ya Kumaliza Kiu Milele?”

“Eee,” akajibu.

“Hupatikana kwa Mungu tu,” wakamjibu.

“Na huyo Mungu yuko wapi?” akauliza.

“Si yuko Mbinguni-duniani,” wakamwambia (uk.38-39)

Jambo hili linamshangaza sana kwani alielewa fika kuwa atokako ni duniani wala sio Mbinguni. Anaposema kuwa amepotea njia baada ya kuambiwa kuwa huko si Mbinguni, wanamwambia kuwa hakupotea na maadam yuatoka Duniani basi yeye ndiye mwenye habari kuhusu Mwenyezi Mungu. (uk.38-41).

Dzombo anawasisitizia na kuwahakikishia kuwa duniani hakuna Mungu bali kuna miungu wengi yaani wafalme, marais, madikteta na watawala ambao huongozwa na Mungu mmoja ambaye ni ‘PESA.’ (uk.82) Dini hii ndiyo iliyotumika kuwapumbaza watu ili wazidi kuwanyenyekea watawala.

Wawalenisi pia walifikiria kuwa Dzombo ndiye aliyetabiriwa kuwa angefika kule Walenisi akiwa ametumwa na Mungu na basi alipofika huko walidhani kuwa ndiye yule aliyekuwa akitarajiwa (uk.45-46).

Mtataruku huu unaotokea inadhihirisha maoni ya mwandishi kuwa hakuna anayejua aliko Mungu. Lakini kulingana na jinsi alivyosawiri dini na pia kuonyesha ile sehemu ya Sala ya Bwana inayosema kuwa mapenzi ya Mungu yatendeke Duniani kama yatendekavyo Mbinguni, tunaweza kukisia kuwa kulingana na mwandishi Mungu wa kweli hupatikana tu pale ambapo pana usawa, hakuna udhalimu, ubinafsi au ukatili wa aina yoyote ile. Hii ndiyo sababu

iliyompelekea Dzombo kufikiri kuwa Walenisi ni Peponi kwani hakuona yeyote aliyekuwa na tatizo lolote lile liwe la lishe, mavazi, elimu au ukosefu wa kazi.

HITIMISHO

Katika sura hii tumeona jinsi ambavyo mwandishi wa riwaya ya *Walenisi* ameisawiri dini. Kwa kiasi kikubwa ameionyesha dini kama kasumba inayompa mtu mnyonge tamaa ya kesho nzuri huko Mbinguni na kumfanya asipiganie haki na usawa duniani. Ameonyesha jinsi dini inavyoweza kutumiwa kuwadhulumu watu.

Anaona kuwa dini hizi zililetewa Waafrika ili wageni wenyewe waweze kuwadhulumu wenyeji huku wakisingizia kuwa ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Waafrika wawe watu 'wasiobahatika.' Kwa upande mmoja, Mkangi hazithamini dini kabisa na kuonyesha dhahiri kuwa hazifai bali zinafaa kupigwa marufuku ili wanyonge wajinasue kutokana na kasumba zao zinazopumbaza na kuweza kupigania haki zao kwa ukakamavu. Katika riwaya ya *Walenisi*, ni dhahiri kuwa jamii ya ulimwengu uliosawiriwa, yaani Wawalenisi hawakujali dini sana bali walianza mfumo uliosisitiza usawa na utu na huku wote wakipendana na kuheshimiana bila kujali umri, cheo au jinsia ya mtu. Mwandishi ameonyesha jinsi watawala dhalimu wanavyotumia hata maandiko matakatifu kuwadanganya wanyonge. Pia ameonyesha mtafaruku uliopo kuhusiana na swala la aliko Mungu, Wawalenisi wanadhani kuwa Dzombo ametoka kwa Mungu, naye anadhani kuwa amefika kwa Mungu.

Kwa upande mwingine, mwandishi ametumia mafunzo ya dini, kama vile Sala ya Bwana iliyoko kwenye Biblia kuonyesha kuwa wanyonge lazima wafunue macho na kuelewa mafundisho ya dini bila kutegemea fasili za watawala ambao huifasili tu kulingana na matakwa yao ya kibinafsi. Mwandishi basi anaonyesha kuwa dini ikieleweka na kutumiwa ipasavyo inaweza kuleta

mabadiliko mema katika jamii. Katika majadiliano yake na C. Mwitia, mwandishi alisema kuwa dini ina msingi ya kutufundisha kuwa watu bora na kutufundisha nidhamu, kwa hivyo anaona kuwa dini bado ina nafasi katika utawala. Okullu (1974 na 1984), ameyonesha kuwa dini ina nafasi muhimu katika siasa na utawala wa nchi, ingawa ameegemea zaidi kwenye dini ya Kikristo. Anasema kuwa dini inafaa kupinga kabisa mambo yasiyofaa yanayotendwa na watawala lakini wakati mwingine wanadini huunga mkono mambo yasiyofaa. Anasema kuwa dini ina jukumu kubwa sana katika kulainisha watawala ili wasiyaendeleze mambo yasiyopendeza kama vile ufisadi na mapendeleo.

Mazingira alimokuwa mwandishi huyu, ya kisiasa, kihistoria na kiuchumi pia yalimwathiri sana katika kuiandika kazi hii. Katika miaka ya themanini, aliwahi kufungwa jela kwa vile aliupinga mfumo wa kiuchumi na kisiasa uliokuwepo nchini katika nyakati hizo. Vyombo vya dola kama vile sheria na polisi vilitumiwa kuyahifadhi maslahi ya tabaka lililotawala. Mwandishi basi ametumia muktadha wa kihistoria kumulika masuala mapana yanayoihusu jamii yake na ile pana ya ulimwengu. Kwa njia hii anadhamiria kumhimiza na kumjasirisha msomaji wake kuyafungua macho kuyaangalia mazingira yake ya kisiasa, kiuchumi na kijamii kwa jicho la ndani, akizingatia yale yasiyosemwa kwa uwazi ambayo yamefumbwa. Riwaya hii pia inadhamiriwa kuwahamasisha wanyonge kujikomboa ili paweze kujengeka jamii mpya yenye usawa, katika viwango vya kitaifa na kimataifa. Wanyonge basi hawapaswi kunyamazishwa kwa chochote kile hasa dini katika vita vyao dhidi ya udhalimu ili ndoto yao ya usawa na utu bora itimike.

Sio tu K. Mkangi aliyeshughulikia asasi ya dini kama ambayo hutumiwa vibaya na wengi. Wole Soyinka, katika tamthilia ya *Masaibu ya Ndugu Jero* iliyotafsiriwa na A. S. Yahya, anaonyesha jinsi viongozi wa dini huitumia kwa njia isiyofaa. Hapa tunakutana ma mhusika mkuu Jeroboam

(Ndugu Jero) ambaye kazi yake in Uaguzi, yaani kufasiri ndoto za watu. Katika tamthilia hii, kuna mhusika aitwaye Chume ambaye ana mke aitwaye Amope. Chume amekuwa akimwomba ruhusa Ndugu Jero ya kumchapa mkewe lakini Jero anamkataza na kudai kuwa Mwenyezi Mungu amekataa hayo.

Yeye mwenyewe Jero anasema:

“Kama mwanafunzi wangu mzuri Ndugu Chume. Anataka ampige mkewe, lakini sitamwachia. Nikimwachia, moyo wake utatua, na itakuwa mmoja katika wafuasi wangu nitamkosa moja kwa moja. Kwa muda ambao yeye ataendelea kutompiga, basi atakuja hapa na moyo haujamtua, na kwa hivyo haitampitikia kutaka kunigeukia. Kwa hakika kila kitu kimepangwa kwa mpango.” (uk. 14)

Kabla ya hapa tunaelezwa kuwa Jero alikuwa amepangisha nyumba ambayo hakuwa ameilipia kwa muda fulani. Baadaye anagundua kuwa mwenye nyumba ni mke wa Chume na anabadilisha nia yake na kumwambia Chume amchape mkewe. Chume anapogundua kuwa Ndugu Jero ndiye aliyekuwa akidaiwa kodi ya nyumba na mkewe, Amope, anakasirishwa sana na jambo hilo na hata baada ya kuidhinishwa na Mwaguzi Jero amchape, hafanyi vile. Hii ni kwa sababu aligundua kuwa Jero ameitumia fursa hiyo kwa manufaa yake mwenyewe, kwani alijua kuwa Chume akimchapa mkewe basi mkewe hataendelea kupiga kambi nje ya nyumba yake akidai kodi.

Mwaguzi Jeroboam pia wakati mwingine anampata mtu fulani akitoa hotuba. Fikira zinamjia kuwa ameshampoteza Chume kwani alidhani kuwa keshampiga mkewe na kuituliza roho yake na hivyo basi hangehitaji Uaguzi wake tena. Basi anaona kuwa mtu yule aliyekuwa akitamani kiti cha uwaziri angekuwa windo lake kwa urahisi. Basi anamzungumzia mtu huyo. Ingawa

anasutiwa na Mbunge huyo, Jero hatikisiki na kumwambia kuwa aliona yule mtu ndotoni akiwa Waziri wa Vita ambacho ni cheo kikubwa kilicho na madaraka. Anajifanya kuwa anaweza kumwomba Mola amwondoshee jukumu lile kwani yeye si mcha Mungu.

Hivi anaivuta nadhari ya yule Mbunge anayeishia kuyasadiki maneno hayo na ananyanyua mikono juu kama ishara ya kukubaliana na Jero.

Kutokana na mifano hii, tunaona jinsi ambavyo Ndugu Jeroboam anavyoitumia dini ya Kikristo kujinufaisha yeye mwenyewe huku akiwadanganya wafuasi wake kuwa anayowaeleza yameteremshwa moja kwa moja kutoka kwa Mola mwenyewe. Ni dhahiri kuwa kwa kutiwa woga na Mwaguzi Jero, yule mbunge angekuwa radhi kumtimizia Jero lolote lile bora tu amwombee na kuendelea kumtabiria Uwaziri na vyeo vikubwa vikubwa.

4.0 DINI KATIKA RIWAYA YA *BABU ALIPOFUFUKA*

4.1 UTANGULIZI

Katika riwaya hii mwandishi ameonyesha jinsi viongozi na watu wenye uwezo mkubwa wa kiuchumi na kisiasa wanavyoweza kuidunisha dini na hata kujiona kama wao ndio viumbe wa kuabudiwa. Hivyo basi anaonyesha kuwa jamii ya kisasa haioni maana ya dini kama ile iliyokuwapo hapo mbeleni ambapo watu waliienzi dini na hakuna aliyedhubutu kujitoshanisha na Mungu au kiumbe aliyeabudiwa katika dini fulani kwani haya yangechukuliwa kama kukufuru.

4.2 TASWIRA YA DINI KATIKA RIWAYA

Kwa kiasi kikubwa, dini katika riwaya hii inajitokeza kutokana na kutajwa kwa **Proteus**. Kunaweza kuwa na fasili nyingi za jina hili lakini tumelichukulia katika muktadha wa dini. Jukumu letu ni kuonyesha jinsi jina hili lilivyotumika hapa.

Kulingana na *Encyclopaedia Britannica* (2003, Juzuu la 9: 741) **Proteus** ni mwanamume mzee wa baharini aliye na unabii, yeye pia ndiye huchunga viumbe vilivyo baharini. Yeye alikuwa chini ya himaya ya Poseidon, mungu wa baharini na aliishi kwenye Kisiwa cha Phoros, karibu na mwanzo wa Mto Nile au katika Kisiwa cha Carpathus kati ya Crete na Rhodes. Alijua mambo yote – yaliyopita, yaliyopo na yajayo – lakini hakupenda kusema aliyoyajua. Wale waliotaka kupata ushauri wake iliwabidi wamshike na kumfunga vyema wakati wa usingizi wake wa adhuhuri. Hata anaposhikwa angejaribu kutoroka kwa kujibadilishabadilisha hali mbalimbali. Lakini mshikaji wake akimshika vizuri basi Mungu huyu angerudia hali yake halisi na kupeana

jibu lililohitajika na kujitumbukiza majini. Kutokana na nguvu zake za kuchukua hali aliyoitaka,

Proteus alichukuliwa kama ishara ya kilichotumiwa kuumba ulimwengu.

Katika *Encyclopaedia of Religion* (1987, Juzuu la 13: 223) **Proteus** ni mungu wa Kiyunani aliyekuwa na kipawa cha unabii na aliulizwa mara kwa mara kufichua yajayo katika maisha ya mtu. Kama kusisitiza kwa waliosaka msaada wake ule uchungu unaotokana na funuo hizo. alijibadilishabadilisha na kuwa kiumbe wa kutisha ili kuwaogofya hao. Kwa wale waliokataa kutishwa naye aliwajulisha walichokitaka kujua.

Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*, tumeelezwa kuhusu K, mhusika mkuu. Tumeelezwa jinsi alivyokuwa mkwasi kupindukia, ana jumba kubwa ajabu, gari aina ya **limonsin** na kazi nzuri. Mbali na haya, wameachana na mke wake na badala yake amempatia upande mmoja wa jumba lile anamoishi na wana wao wawili, Kidawa na Bamkubwa. K anaishi na jibwa lake *Doggy* linalopewa chakula kama binadamu. Chakula cha jibwa hili kinatoroshwa na mzuka anayeona kuwa kinafaa kuliwa na wanadamu wanaokufa njaa na sio jibwa. Huyu K kwa sababu ya ukwasi wake, wakati mwingine hujihisi kama yeye ni mungu wa aina fulani. Tunaambiwa:

“Na K zaidi ya wote, anaamini kwamba watu wote lazima waamini kama anavyoamini yeye kuwa hakuna mbora mwingine zaidi ya **PROTEUS**. Hata Proteus akiingia gizani kujificha, akatafutwe kuombwa kuja kuleta uwokozi katika kila jambo. Na kwa kweli si amewasikia mara ngapi watu wakiungama kwamba hawajui wangepanya nini iwapo Proteus atakufa leo. Na yeye K hujibu moyoni mwake, ‘Mimi nitakuwa **Proteus** wa pili,’ Ingawa hata yeye K anajua kwamba Proteus hawezi kufa. Anaweza kujigeuzageuza tu. Kwa kweli mara ngapi

mwenyewe **PROTEUS** amesema hafi? Anaweza kuwa mti mkubwa badala ya Bahari ya Hindi...” (uk.11)

Kutokana na dondoo hii tunapata kuwa K akiwaza kuhusu **Proteus** (mungu) anaona kuwa hakuna mwingine mzuri zaidi yake na anaendelea kuwaza kuwa kama **Proteus** angekufa yeye ndiye angekuwa **Proteus** wa pili. K ni mmojawapo wa watu wale waliotajirika zaidi ambao mwandishi anasema haya kuwahusu:

“Husema hivyo huku moyoni mwake kajaa fahari na kujipongeza namna gani anavyojua kwamba wameshazikanyaga chini ya nyayo zao roho na akili za watu wao milele. Kwamba vichwa vya watu wao havishiki tena hata kwa yale yaliyopita jana, seuze juzi! Sahau ... ugonjwa mkubwa sahau, unaowapa faida wao kuendelea kukuza miti na kutaka kuruka juu kugusa mbingu bila ya mbawa. Sahau ya watu ambao hawakumbuki tena fedheha wala aibu, unyonge wala ufukara! Hawakumbuki hata kama wao ni watu tena. Na kwa hivyo, wakati wote huo tokea zamani, wao **ukofiwatu**, wamekuwa wakisimama kutaka kujua nini watu wote wanataka – wao wenye idadi isiyozidi vyanda vya mikono. Na wanavyotaka wao ukofiwatu ndiyo lazima yawe.” (uk. 11)

K ni mmojawapo wa hawa ukofiwatu (watu wa chache wanaowakalia wengine juu, watu ambao wingi wao ni wa kujaa kiganjani tu, uk.171). Hawa ni viongozi wa kisiasa ambao hawathamini watu wa kawaida kwa sababu ya kuwa kwenye tabaka la juu zaidi kisiasa na kimali. Hii ndiyo sababu inayomfanya K, kujiwazia kuwa hata **Proteus** (mungu) akifa yeye atakuwa **Proteus** wa pili.

Pia tunapata kuwa huyu K haithamini dini na sala zake bali yeye huenda kusali kama desturi tu wala sio kutokana na msukumo wowote wa kiroho. Tunaambiwa:

“K alijitayarisha kuvaa kiijumaa: chupi fadhili, kikoi, bulbul, fulana ya msewe laini, kanzu, darzi ya kitambaa maalum, koti la lasi asilia, kofia barghashia, na miguuni kubadhi la haja. K husali sala moja kwa wiki, na sala hiyo kila siku alihakikisha anawapa mkono watu wengi inavyoyumkinika.” (uk.65)

Hapa tunaona kuwa K ni kama anayachukulia mavazi kama ndiyo yanayoonyesha uwanadini wa mtu. Yeye hufanya sala moja peke yake siku ya Ijumaa. Kwa hivyo hili ni kama jukumu lililosukumizwa kwake bila yeye kutaka na ndio analichukulia kama la kidesturi tu ndio awaridhishe wengine.

Wakati K na mzuka walipoenda safari ya chini ya ardhi, akiwa katika ulimwengu ule mwingine uliojaa watu maskini ambao walipita tu sokoni wakitazama bidhaa zilizokuwa zikiuzwa na kushindwa kuzinunua kwa ukosefu wa fedha na ughali wa bidhaa zile, wale watu wanamwona K kama mungu (**Proteus**) wa aina fulani. Tunaambiwa:

“Wengine walipompita na kumwona K walisita na kusitisha kauli zao hizo... wakasimama tutwe na kumchuja K tokea juu mpaka chini na kisha wakamwita huku wakitoweka, “Protausi,” (kwa maana ya **Proteus**).

Kutokana na dondoo hii, tunaona kuwa maskini huwachukulia wakwasi kama miungu kwa sababu ya ule uwezo wao kiuchumi na kisiasa. Ni kama hawaoni kama kuna kiumbe mwingine aliye na nguvu zaidi kuliko wakwasi au viongozi hao na wanaona ni kama hawa ndio walioshikilia maisha yao duni na ndio maana hata wanatoweka kutoka machoni mwao.

Pia K akiwa kule kwa nyanyake Maajuza alikopelekwa na mzuka, ndugu yake K aitwaye Juba anapoambiwa amvalishe nguo kwani K alikuwa ameibiwa vyake vyote, wote wanatilia shaka jambo la K kuwa kijikuu cha Maajuza. Huyu anasema:

“Kweli! Sasa nakumbuka kwamba K kijukuu chetu tulikipeleka dunia nyengine. Awe **Protausi** na tulijua hatarejea hapa mpaka atakapokuwa tena na haja na sisi.”
(uk. 107)

Inaonekana kuwa kulingana na watu hawa yeyote ambaye ana uwezo uliokithiri kiuchumi alihitimu kuwa Mungu na ndio maana huyu anasema kuwa walimtuma dunia nyingine ili akawe Mungu. Pia anaonyesha kuwa miungu wa aina hii hawawathamini watu wa kawaida bali huwatafuta tu pale wanapowahitaji labda kwa kutaka kura zao.

K akiwa kule kule chini ya ardhi, anafika mahali ambapo pana vibanda vilivyojengwa kwa maboksi, majani, madebe, mabati, miti, alizukiwa na harufu ya uvundo mkali akaziba pua. Kwa sababu ya kitendo hiki chake, Mzuka anamwambia:

“Ha, ha, ha, hakika wengi wenu mmepoteza hata hisia ya kupima uwongo na ukweli uko wapi. Mnangojea kusemewa na **Proteus...**” (uk.128)

Hii inamaanisha kuwa watu duniani wameacha kujishughulikia wao wenyewe bali wamewaachia miungu majukumu yote na ni kama miungu hawa wameshindwa na majukumu hayo na ndio maana umaskini, uchafu na uvundo umejaa ulimwenguni. Hivi basi mwandishi anaonyesha kuwa ikiwa kutakuwa na mabadiliko yoyote mema duniani, basi lazima waja wenyewe wachukue jukumu la kujibadilishia maisha. Wasikae tu na kungojea miungu wawatengenezee. Hii ni kwa

sababu miungu wametengana sana na wanadamu na basi hawawezi wakaelewa vizuri matatizo ya wanadamu.

Pia K akiwa huko huko aliwaona watu wakiwa wanatembea kinyumenyume huku wakiwa wamebeba vibuyu. Hawa wanajipanga nyuma ya majitu marefu yaliyokuwa yameinua vibuyu vikubwa na kuinua vibuyu vyao vidogo. Watu hawa wanachomwa na jua na kunyeshewa na vua kubwa kwa masafa lakini hawayahisi haya yote. Baadaye kulifuka buhuri zito la mvuja, yaani joshi jingi na zito linalofuka la majani au utomvu unaonuka sana, na kutua juu ya vichwa vya watu ambao baada ya muda mfupi walionekana kama waliolewa. Baadaye watu walianza kusukumana na sauti zito lilikuja juu na kuwaambia watu waache kwani Manekineko (paka la Kijapani) kila siku linaita halikimbizi pesa...Gwaru la Tai (la Kimarekani) hunyakua tu, halitoi sadaka na Euro ni ufupisho wa uroho. Tunaambiwa:

“Ghafla, watu waliokuja kughadhibika ghafla walianza kuhujumu kitu au mtu katikati ya umati wa watu. Labda yule mtu aliyewaonya. Kwa namna fulani, K lilimfurahisha jambo hili, lakini hakuonyesha. Hata hivyo, kabla furaha yake haijamshuka maungoni, alishtuka biwi la moshi mkubwa linasimama juu ya vichwa vya watu na kuchukua sura ya umbo la mzuka. Walipoona hivyo watu, walianza kutimka mbio, na kusukumana na kupandana na kuvurugana, na kuumizana na hata kuuana. Waliowahi walitimka mbio bila ya kutazama nyuma ingawa walisikia sauti za lile kundi la mijitu iliyosimama mbele ikiwaita:

‘Rudini, hakuna kitu... Hakuna neno rudini... Rudini nyiyewoga...’

Walikimbia maili kadha pale penye nyika. Mbele zaidi wakapunguza kasi. Walikuwa taabani wamechoka. Pumzi juujuu zinawafoka. Mara wakajikuta wanagawika mapande. Kila upande ukaanza kuutupia mwengine mawe ya dini.

‘Nyinyi...’

‘Hapana, ni nyinyi...’

Askari wa Fanya-Fujo-Uone wakazuka ghafla. Na lo!” (uk.131)

Katika dondoo hii, tunaona jinsi watu hawa walivyokuwa pamoja pale walipokuwa wameinua vile vibuyu vya kuomba msaada. Baadaye kunatokea moshi mzito kutoka juu na kuwafanya watu hawa kuwa kama punguani. Baada ya muda wanagawika katika mapande na jambo lililo dhahiri ni kuwa mapande yale yalikuwa ni katika misingi ya kidini. Mwandishi anaonyesha kuwa dini huwagawa watu na kuwafanya wadhulumiane katika misingi hiyo. Watu wanaishia kulaumu wale wasio wa dini yao na mwishowe inabidi wanyamazishwe na askari.

Pia yale masanamu ya Manekineko, paka wa Kijapani, Tai la Kimarekani na Gwaru la Euro, ni kama miungu wa aina fulani kwa vile wanaombwa misaada na watu lakini kama inavyojitokeza ni wazi kuwa hawa hawana msaada wowote kwa waombaji wale kwani tunaambiwa:

“...Manekineko kila siku linaita halikimbizi pesa... Gwaru la Tai hunyakua tu, halitoi sadaka. Na Euro ni ufupisho wa uroho...” (uk.131)

Hivyo basi hawa wakichukuliwa kama miungu, inaonekana kuwa hawana umuhimu wowote kwa waja kwani lao tu ni kudhulumu na kuwafisidi watu.

Baada ya K kurudi kutoka ile safari yake ya kiakili aliyopelekwa na mzuka alirudi ofisini mwake na kupata rundo la majalada yakimngojea. Pia alipata barua katikati ya meza iliyoonyesha kwa hati ya juu ya bahasha kuwa ilitoka kwa **Proteus**; alishuku kitu na hata hakuisoma. Anawaza tu kuwa Proteus hajapata kumwandikia barua bali humpigia simu anapomhitaji. K alijiuliza,

“Kuna uhusiano gani baina ya barua ile na yale yanayotokea?” (uk. 157)

Yale mambo yanayotokea hapa ni kwamba K ameharibikiwa na yote na haya yanadhihirika hata nyumbani kwake ambapo tunaambiwa kuwa hakuna maji, hata bwawa limekauka, umeme umekatwa na wafanyikazi wake hawajalipwa kwa miezi sita. K mwenyewe anakiri kuwa sababu ya wafanyikazi wake kutolipwa kwa muda wote huo ni kuwa:

“Hakuna fedha...” (uk.158).

Karani wake anayafuasa maneno haya ya mkubwa wake kwa kejeli kwani hakuamini kuwa mtu mkwasi kama K anaweza kukosa fedha namna ile. Vile vile kuna sauti inayomwambia aisome ile barua lakini anakataa kuisoma. Hapa ni kana kwamba ashajua kuwa Proteus hamtakii mema katika ile barua. Pia inaonekana kuwa yeye hayathamini mambo ya miungu kwani anaona kuwa wao ni wasumbuaji wasiowatakia waja mema.

Pia jioni alipoenda katika hoteli ya **Neo-Casino** alikozoea kwenda na wakwasi wenzake wenyeji na wageni, kama vile Delpiero, Miyazawa, Von Heim, Di Livio, Bw. Sungura, Bw. Mbomba na wengine, alipata kuwa kule pia mambo yamemtumbukia nyongo. Ingawa alipiga simu kuwaarifu kuwa anaelekea huko, hakuna aliyemlaki kama ilivyokuwa kawaida. Isitoshe alimwona kimada wake, Zuhura Mapozi, akiwa amekumbatiwa na rafikiye mkubwa Bw. Tajuri, bintiye pia alikuwa mle akicheza densi na rafiki ya babake, Bw. Miyazawa. K alipojaribu kuingia humo ndani alizuliwa na walinzi wanne wanaomwambia kuwa wana amri ya kutomruhusu kuingia mle. Baada ya kuyashuhudia yale yote tunaambiwa:

“Sasa yaliyomo ndani ya barua yalikuwa wazi kabla hajaisoma.” (uk.160)

Baada ya haya tunaambiwa kuwa K hakustahimili tena bali aliingia uwanjani kwa fujo huku akimtusi kila mtu, hata **Proteus** (uk.163)

Anaporudi kasrini mwake akiwa majinuni, anapata kuwa mambo yameharibika zaidi. Anapoifungua ile barua aliona kuwa amenyang'anywa madaraka, na tena arejeshe vitu vyote vya serikali na pia serikali itachukua mali yake yote kulipa madeni anayodaiwa. Siku ile ile saa moja jioni askari walikuja na kumwambia kuwa amepewa masaa mawili pekee atoke kasri lake kwani limepigwa tanji kufidia madeni anayodaiwa na serikali na watu binafsi. **Limonsin** pia anaambiwa aliache. Pia tunaambiwa kuwa wakati ule mkewe alikuwa amesharudi kwao baada ya kuugua wazimu wa unyamavu na wanawe hakujua walikuwa wapi. Isitoshe nje ya kasri lililokuwa lake kuliwekwa jeshi zima kulilinda ili K asithubutu kurudi ndani. K pia anashikwa na wazimu unaomfanya avue nguo zake zote, jambo linalosababisha kuchekelewa kwake na watu wote. Ilimbidi Biye ampeleke K kwao kwa Bi. Maajuza. Tunaambiwa kuwa aliporudi kule kwao kijijini mambo yalizidi kuharibika na hakulala usiku kucha. Alipiga kelele zisizoeleweka na yeyote na alimtaja **Proteus** kila wakati. Alisema:

“Wewe ni nani hasa **PRO-TEUS**? N'najua wewe si Mungu lakini kwa nini nguvu zako zinafanana na za ki-Ungu? ... Kwa nini maisha ya kila mtu yawemo mikononi mwako? Kwa nini kisirani chako hakiishi? Kwa nini tumekuwa tukikuamini muda wote huu, na bado waliobaki wanakuamini? Kwa nini umeikata ndoto yangu? Kwa nini umeifisidi haki yangu ya kuishi? Kwa maslahi ya nani umeichukua mali yangu? Nani anayetnonoka na mipango yako? **PROTEUS... Proteus... Proteus...**” (uk.165)

Kama tulivyoielezwa hapo juu, Proteus ni mungu mmojawapo wa miungu wengi wa Kigiriki aliyehusika na kuwatabiria waja mustakabali wao. Ingawa yeye si Mungu mkuu alikuwa na athari kubwa na pia nguvu za mamlaka ya kiasi katika maisha ya wanadamu. K anapopatwa na masaibu hayo yote anamkasirikia sana Proteus na hata kumuuliza ana mamlaka gani ya kuudhibiti mwisho wa watu. Pia anaona ni kama Proteus ameifisidi haki yake ya kuishi na kuchukua hata mali yake.

Anamuuliza pia ni nani anayeweza kukaa na kufurahia mipango yake ambayo kulingana na K imejaa usumbufu mtupu. Mwishowe K, kwa kuzidiwa na yote na kwa kule kukosa matumaini ya kusaidiwa na Proteus, anajitia kitanzi na kujiua. (uk.165)

HITIMISHO

Kwa kuhitimisha kuhusu dini katika riwaya hii, tunaweza kusema kwamba viongozi na watu wenye hali na mali hujichukulia kama wasiogusika na Mungu au miungu. Wao huwa wamekengeushwa na maisha ya mjini yanayowatononosha na kuwafanya wasahau kuwa kuna kiumbe au viumbe walio na nguvu na mamlaka juu ya maisha yao. Wao hujiona kama wanaotoshana na viumbe wale na hata kuwafanya wengine wasadiki kuwa wao ni miungu wa aina fulani kama tunavyoona Bi. Maajuza akisema kuwa walimtuma K dunia nyingine akawe Protausi (**Proteus**). Wao hujihusisha na mambo ya dini kwa sababu ni desturi tu kwao bali sio kwa hiari yao. Tunaona kuwa K anatilia maanani mavazi ya kidini na kutoa zaka kuliko yale yanayotendeka katika vyumba vya ibada. Pia kwa sababu ya kukengeuka kwao, wanataka hata kuanzisha mradi wa **FKK** uliohusu watu kuingia mahali fulani wakiwa uchi. Jambo kama hili haliwezi likakubaliwa na dini kwa vyovyote vile. Watu kama hawa wanapoharibikiwa na maisha huishia kumlaumu kiumbe mwenye mamlaka juu ya mustakabali wao huku wakisahau maovu yao. Kwa hivyo mwandishi anaonyesha kuwa watu wakiwa na uwezo mwingi wa kiuchumi na hata kisiasa hawaithamini dini kamwe kwani wao hujiona kama miungu pia miongoni mwa akina yakhe. Hivi basi dini haina umuhimu wowote kwao kwani wanaona kuwa wamejitosheleza kwa vyote.

Tukilinganisha na riwaya ya *Walenisi* kuna Wachuna waliokuwa wakwasi kupindukia na walijichukulia kuwa viumbe walioumbwa na Mungu mahususi wakiwa na akili nyingi zaidi na pia wawe na uwezo mwingi wa kiuchumi kuliko wachochole waliowaita wasiobahatika.

Maskini nao huitumia dini kujigawa katika makundi. Wakati K alipokuwa akitembea chini ya ardhi alikopelekwa na mzuka, aliwaona watu walioinua vibuyu juu kuomba msaada.

Waliokuwa wengi (mamilioni yao: uk.130), walikuwa maskini wategemeaji wa misaada na wachache (darizeni moja: uk.130), wakawa ni majitu manene yanayotaka tu kujitajirisha zaidi.

Baada ya kupatwa na kichaa cha aina fulani, wale maskini walitoroka na kusihiwa warudi na kundi la majitu lililobaki pale pale likisimama, walijigawa mapande na kuanza kurushiana mawe ya dini, yaani kudhulumiana kwa misingi ya tofauti zao za kidini. Hivyo basi hawaoni thamani ya dini isipokuwa tu kuitumia kujigawa na kudhulumiana wenyewe kwa wenyewe.

SURA YA TANO

5.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 HITIMISHO

Katika kazi hii tumetumia nadharia mbili ambazo ni Uhalisia na Umaksi. Kwa kuzingatia nadharia ya Uhalisia, mwandishi wa kazi yoyote ile ya kifasihi anafaa, kwa kiasi kikubwa, kusawiri hali halisi ya maisha katika jamii-husika. Anafaa atumie wahusika wa kawaida au wanaoweza kupatikana katika jamii halisi na kuyachunguza na kuyasimulia maisha yao na tajriba zao na kuonyesha mandhari na mazingira ya kawaida. Mwandishi anapaswa kusawiri vilivyo maisha ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kitamaduni ya jamii – husika. Katika tapo hili hakupaswi kuwa na uajabu au ufantasia wa aina yoyote, bali vyote, yaani mandhari, mazingira na wahusika vinapaswa kuwa halisi kama katika ulimwengu halisi. Picha na yaliyomo katika kazi hizi yanafaa kuwiana na ukweli na uhalisi wa jamii zinazohusika.

Katika sura ya pili, tumezingatia taswira ya dini katika riwaya ya *Nguvu ya Sala*. Katika riwaya hii mwandishi ameangalia maswala kadha yanayoonyesha hali halisi ya maisha ya jamii anayoizungumuzia ambayo ni ya Kiafrika. Amesawiri wahusika wa kawaida wanaoweza kupatikana katika jamii halisi na kuchunguza na kusimulia maisha na tajriba zao. Pia ameonyesha mandhari na mazingira ya kawaida. Hakutumia ufantasia wa aina yoyote. Hivi basi kazi hii yake inaafikiana na matakwa ya nadharia ya Uhalisia.

Katika kazi hii ameyasawiri maudhui kama vile dini na kizazi kipya, dini na utamaduni, dini na malezi ya watoto na dini kama imani isiyo na mashiko. Mwandishi, kuhusiana na dini na kizazi kipya, ameonyesha jinsi vijana wanavyoyachukia mambo yahusianayo na dini. Haya ni kupitia

kwa mhusika mkuu Richard ambaye tunaambiwa kuwa, walikuwa wakihudhuria mikusanyiko ya dini, yeye na vijana wenzake, wa kike na kiume na kukaa nyuma ya kanisa huku wakipiga kelele. Mwishowe walitoka nje wote pindi tu mahubiri yalipoanza. Pia vijana walipendelea sana kufurahia vitamu vilivyopeanwa kanisani wakati wa Krismasi bila kutaka kuelewa maana yake. Haja yao tu ilikuwa kujifurahisha.

Mwandishi pia ameonyesha jinsi mara nyingi utamaduni na imani za jamii-husika zinavyoshinda imani za kidini na kuzionyesha kuwa zisizo na nguvu zozote zile. Pia mwandishi ameonyesha jinsi malezi ya watoto yaliyokitwa katika misingi ya dini pekee yanavyofeli. Haya ni kupitia kwa mhusika Richard ambaye anasisitiza tu mafundisho ya dini na nguvu ya sala bila kuwaelekeza wanawe katika maisha halisi. Kutofaulu kwa malezi haya kunajitokeza wakati mwanawe wa pili, Roselyn, anapopata mimba akiwa katika kidato cha pili. Susan, mwanawe wa kwanza pia hakupendezwa na malezi ya aina hiyo na ndio maana akamzungumzia babake kuhusu ubaya wa malezi ya aina hiyo.

Mwandishi pia ameonyesha kukubaliana na mawazo ya Sigmund Freud (1961) aliyesema kuwa dini ni imani isiyo na mashiko. Mwandishi ameonyesha haya hasa kupitia kwa yule mhubiri kule *Uhuru Park*. Huyu kupitia kwa maneno yake ya kuwanasihwa watu wampe Mungu maisha yao anaonyesha dhahiri kuwa wanaopaswa kujihusisha na dini ni wale walio na matatizo chungu nzima kuonyesha kuwa dini ni ya kuleta mliwazo tu. Aidha, ameegemea zaidi katika dhana ya udhanaishi na kuonyesha jinsi maisha hayana maana, ni usumbufu mtupu, hasa kupitia kwa mhusika mkuu Richard. Richard anasumbuka sana kuanzia utotoni mwake hadi katika utu uzima anapooa mke ambaye keshabikiriwa na mwanamume mwingine na kutiwa mimba. Familia ya Richard pia ina masumbuko mengi sana. Watoto wanachapwa kinyama kwani makosa hata

madogo yanawekewa misingi katika dini. Mwandishi huyu basi ameonyesha kuwa hakuna haja ya watu kutia imani yao katika dini kwa kuwa ni imani potofu na haina suluhisho lolote na hivi basi wanadamu wanapaswa kujitegemea wao wenyewe sio kungojea msaada kutoka kwa viumbe wenye nguvu kuwashinda.

Katika sura ya tatu tumeangalia taswira ya dini katika riwaya ya *Walenisi*. Hapa tumeona kuwa mwandishi ameyamulika mambo mengi halisi kama vile matumizi mabaya ya dini na wanasiasa ili kujinufaisha wenyewe na pia watu maskini kunyamazishwa kwa kutiwa tamaa za maisha mema ya baada ya kufa kwao. Mwandishi anaukwepa uhalisi kwa kiasi ili kuusawiri ulimwengu-kielelezo ambao kulingana naye unaweza kuletwa tu na hali ya kiuchumi ya ujamaa. Hivi basi anatumia mwelekeo wa kifantasia kuonyesha ulimwengu usio na njaa, vita, dhuluma, maonevu wala ubinafsi. Huzuni na furaha ya mmoja huwa ni ya wote. Kwa hivyo kulingana na mwandishi uhalisia wa ujamaa sio jambo gumu kutekelezeka, bali unahitaji juhudi, elimu iliyo na manufaa na utafiti ambao unaleta masuluhisho kwa matatizo yanayowakumba wanajamii kwa jumla. Mwelekeo wake basi katika ufantasia ni wa kusaidia kusisitiza ujumbe wake wa kuutupilia mbali ubepari na kuukumbatia ujamaa. Mwandishi anaona kuwa haya yatawezekana tu ikiwa wanyonge watakataa kuhadaiwa na wakwasi kwa dini kuwa maisha mema yanawangoja baada ya kufa kwao. Maisha mema yasiyo na matatizo yoyote yaweza kupatikana mumu humu duniani, kwa maoni ya mwandishi.

Aidha, mwandishi huyu ameegemea katika nadharia ya Umaksi. Umaksi hupinga kwa kinywa – kipana mafunzo yote ya dini na kuhubiri ukomunisti na ujamaa. Wana-nadharia ya Umaksi kama vile Marx na Engels huchukulia dini kama aina ya muhadarati (afyuni) ambao huwalevya na kuwapumbaza watu na kuwafanya wasijikakamue kujinasua kutoka kwa minyororo ya dhuluma

za watesi wao. Mwandishi ameonyesha jinsi dini ilivyotumiwa na vyombo vya ki-itikadi vya Dola kama vile siasa, elimu na sheria kushindilia dhuluma ya vyombo-kandamizi vya Dola kama vile polisi, magereza na majeshi. Dini iliwalainisha watu na kuwaogofya kwa kuzua Peponi na Jehanamu. Mwandishi anawaunga mkono Wamaksi kuwa maendeleo ya kweli yatapatikana pindi tu athari zote mbaya za dini zitakapoondolewa na ujamaa kuzingatiwa. Mwandishi anaonelea kuwa dini ikitazamwa ipasavyo inaweza kuleta suluhisho, hasa pale anapoitumia *Sala ya Bwana* kama kielelezo cha maisha bora duniani kama yalivyo Mbinguni. Mwandishi pia ameonyesha kuwa dini wakati mwingine inaweza kuwa tatanishi hasa pale anapomsawiri Dzombo akidhani kuwa Walenisi ni Mbinguni nao Wawalenisi wanadhani kuwa yeye ametoka Mbinguni-Duniani kwa Mwenyezi Mungu na kwa hivyo yeye ni mungu wa aina fulani.

Katika riwaya hii, mwandishi ameufumbata uhalisia kwa kutumia mtazamo wa kifantasia ili kuumba jinsi ulimwengu unavyopaswa kuwa, tofauti na ulivyo sasa, kwa hivyo kamwe hajaukwepa uhalisia, ni mtindo wake tu wa uandishi.

Katika sura ya nne, tumeshughulikia dini katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*. Hapa mwandishi ameyamulika mambo ya kihalisia ingawa ni kwa mtazamo wa matukio ya kiajabuajabu. Haya ni kama ile safari ya K walioenda na mzuka ambapo ilibidi ajiue na kuvalia figu la mchwa na kisha wakapitia kwenye mizizi ya miti. Kwa kiasi kikubwa amemulika maisha halisi ya wanadamu, ameonyesha jinsi walio wakwasi kupindukia wanavyokuwa na ubinafsi kiasi cha kutozijali hata jamii zao. K anaishi peke yake na jibwa lake na familia yake inaishi upande mwingine wa kasri lake. Mwandishi ameonyesha jinsi uwezo uliokithiri wa kiuchumi na kisiasa unavyoweza kumkengeusha mtu na kumfanya ajihisi kuwa mungu wa aina fulani. Haya ni kupitia kwa huyu mhusika K anayehisi kuwa hata **Proteus** (mungu) akifa, yeye K atachukua mahala pake kwa

sababu ya ule uwezo wake mkubwa wa kiuchumi na kisiasa. Baadaye anapofilisika anamkasirikia yule mungu na hata kumtukana na kumlaumu kwa masaibu yake yote.

Kutokana na haya yote tunapata pia kuwa nadharia tete zetu zote zimejitokeza kwa njia iliyo dhahiri katika riwaya tulizozishughulikia.

Kwa kuhitimisha tutasema kuwa waandishi hawa watatu wamesawiri hali ya kutamausha ya dini. Wameonyesha kuwa dini imeshindwa kuleta suluhisho kwa matatizo ya wanadamu. Masuluhisho yanayotolewa na dini hayamwelekezi binadamu katika kuyatatua matatizo yake bali anaambiwa aamini tu nguvu ya sala au aweke imani yake katika ahadi ya maisha mema baada ya kufa, yaani huko Mbinguni na hivi basi kuyakubali matatizo yake.

Waandishi hawa aidha wameonyesha kuwa dini haimpatii mwanadamu suluhisho kuhusu maana ya maisha bali inamsawiri mwanadamu kama kiumbe aliyetupwa ulimwenguni usio na huruma na ambapo hakuna Mungu bali binadamu anafaa kuurakibu akiwa peke yake huku akitegemea majaaliwa au Jaala.

Waandishi hawa aidha wameonyesha kuwa dini imeshindwa kuleta kizazi kipya kiadilifu. Vijana wamesawiriwa kama wanaochukizwa sana na mambo ya dini hasa wale ambao wamesoma hadi chuo kikuu. Pia katika *Nguvu ya Sala*, mwandishi ameonyesha kuwa vijana wanaolelewa katika misingi ya kidini ndio wanaokuja kuasi na kupotoka zaidi kama wahusika Roselyn na Bethsheba.

Dini pia imesawiriwa kama asasi inayotumiwa na wanasiasa kuwanyanyasa wachochole kwa manufaa yao binafsi huku wakisingizia kuwa matatizo ya 'wasiobahatika' yanatokana na

mapenzi ya Mola mwenyewe. Katika riwaya ya *Walenisi*, mwandishi pia ameonyesha kuwa dini zilizopo Afrika zililetwa na wakoloni kwa minajili ya kuwanyanyasa Waafrika wenyewe huku wakiwanyamazisha kwa matumaini ya maisha mema Mbinguni na kuwaonya kuhusu kuoneana wivu kwani ni dhambi hasa kulingana na Amri Kumi zilizo katika *Biblia Takatifu*.

Ni kwa sababu ya kuchukizwa kwake na athari za dini katika familia yao, Susan, katika *Nguvu ya Sala* anamtolea maneno makali babake kuhusiana na udhaifu wa mwito wake wa kutegemea nguvu ya sala. Mwandishi anayadadisi na kuyachunguza mambo ya dini kwa jicho la ndani na kuonyesha kuwa ina upungufu fulani.

Kwa kuzingatia haya yote, ni dhahiri kuwa kulingana na waandishi hawa dini imepoteza ile nafasi yake kubwa na muhimu ya hapo awali na hivi basi wanadamu wanafaa kuichuja na kujua ni yapi mema na yapi mabaya katika imani za kidini. Swala la udhanaishi lilitokea baada ya Vita Vikuu vya Pili vya Dunia ambapo kulikuwa na uharibifu mwingi wa mali na umwagikaji mwingi wa damu. Wanadamu walianza kudadisi kama kweli kuna Kiumbe mwema asiye na dosari yoyote na ambaye anatawala na bado kuyakubalia maovu ya aina zote kutendeka duniani.

Msimamo wa waandishi hawa ni kuwa dini imepoteza umuhimu wake kwa kiasi kikubwa kwa sababu watu wengine katika jamii ya kisasa wameidunisha kiasi cha kujifikiria kama miungu wa kuabudiwa. Wengine wameikosea imani kwa sababu ya ule udhaifu wake katika kuleta masuluhisho ya matatizo ya kimaisha.

5.2 MAPENDEKEZO

Tungependekeza kuwa utafiti ufanyiwe riwaya hizi kwa kutumia nadharia zingine kama vile Usasa na Usasaleo. Hii ni kwa sababu kazi hizi kwa kiwango fulani zimeegemea zaidi katika nadharia hizi. Waandishi wa kazi hizi wamedadisi misingi ya miundo ya kijamii, kidini, kimaadili na mitazamo ya kijadi kumhusu binadamu kama kiumbe.

Kazi hizi pia zinamulika mawazo yanayompitikia mhusika mkuu akilini. Katika *Nguvu ya Sala*, kuna mawazo mengi yanayompitikia Richard akilini na yanayomulikwa kwa kirefu. Katika riwaya ya *Walenisi*, mengi yanayoelezwa kwa kirefu yamo katika fikra za Dzombo, kama vile safari kwa sayari, na *Safari ya Utu*. Katika *Babu Alipofufuka*, mawazo ya K yameelezwa kwa kirefu hasa ile safari yake na mzuka ya chini ya ardhi, ambayo ni taswira ya kujisaka kwake.

Ukengeushi pia ni sifa nyingine ya matapo haya. Katika riwaya zote tatu, wahusika wakuu wamekengeuka kwa aina fulani. Richard amekengeushwa na imani yake katika dini hivi kwamba anasahau uhalisia kuwa yuko duniani kwenye wanadamu halisi na sio Mbinguni kusiko na dosari yoyote. K amekengeuka kiasi cha kujihisi kuwa ni mungu, naye Dzombo amekengeuka kwa vile hakubaliani na mifumo mibovu ya kiuchumi iliyo nchini mwao na ni kwa sababu hii anahukumiwa kifo kwa sayari. Dhana ya maana ya maisha pia imeshughulikiwa katika kazi hizi zote.

Haya ni baadhi ya masuala yanayotufanya tuhisi kuwa swala la dini katika kazi hizi lingefaa pia kuhakikiwa kwa misingi ya nadharia hizi za Usasa na Usasaleo.

Pia wahakiki wengine wanaweza kulinganisha taswira ya dini katika riwaya hizi na zingine ambazo hazina mitazamo ya kukatisha tamaa kuhusiana na dini, ili kuonyesha kuwa sio wakati wote dini huhusishwa na mabaya tu, kwa mfano, kazi ya Z. Burhani ya *Mwisho wa Kosa* inadhihirisha kuwa dini ina umuhimu na jukumu fulani hasa katika maisha ya ndoa.

Kutokana na mipaka na wakati tuliokuwa nao wa kuandika tasnifu hii, tumejibana zaidi katika yale mambo muhimu yanayojitokeza wazi kuhusiana na dini katika riwaya hizi. Hivyo basi tungependekeza watafiti wengine wazifanyie kazi hizi tahakiki kwa undani zaidi na kuhakikisha kuwa hakuna yaliyoachwa nyuma ambayo waandishi walitaka kuyapitisha katika dhamira, maudhui na fani zao.

Swala la fani pia hatukulishughulikia kwa undani isipokuwa tu pale limehusiana na swala la dini na tungependekeza lifanyiwe tahakiki kamili.

Pia tungependekeza kuwa wahakiki wengine wa kazi kama hizi ikiwezekana wazungumze ana kwa ana na waandishi wenyewe ili waweze kuelewa vizuri zaidi dhamira kuu za wandishi hao na hivi kuweza kuzifanyia kazi hizo tahakiki kulingana na jinsi mwandishi alivyodhamiria.

MAREJELEO

- Abrams, M.H. (1971) *A Glossary of Literary Terms*. 3rd Edition. New York: Holt, Rinehart and Winston, Inc.
- Andala, M. (2003) *Mwongozo wa Walenisi*. Kakamega: Lurambi Publishers.
- Arege, T.I.M. (1998) *Ushairi Huru wa Kiswahili: Mchango wa Euphrase Kezilahabi*.Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.
- Brome, V. (1978) *Jung*. London: Macmillan London Limited.
- Burhani, Z. (1987) *Mwisho wa Kosa*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Coser, L.A (mhar.) (1963) *Sociology Through Literature*. London: Prentice-Hall International, Inc.
- Encyclopaedia of Religion* (1987) Juzuu la 13 Mircea Eliade (Mha) New York: Macmillan Publishing Company.
- Escarpit, R. (1971) *Sociology of Literature*. London: Frank Cass & Co. Ltd.
- Franz, M. L.V.(1975) *C.G. Jung: His Myth in our Time*.London: Hodder and Stoughton Ltd.
- Freud, S. (1961) *The Future of an Illusion*. New York: W.W. Norton & Company Limited, Inc
- Gatare, J.K. (1993) *Dini katika Riwaya za Kezilahabi*. Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.
- Gehman, R.J. (1993). *African Traditional Religion in Biblical Perspective*. Narobi: East African Educational Publishers.
- Heinemann, F.H. (1950) *Existentialism and the Modern Predicament*. New York. Harper and Brothers
- Hoffman, J. (1975) *Marxism and the Theory of Praxis*. London: Lawrence and Wishart.
- Hornby, A.S. (1998) *Oxford Advanced Learners Dictionary*. New York: Oxford University Press.

- Johnson, F. (2003) *English-Swahili Dictionary*. Nairobi: Oxford University Press.
- Kayongo-Male, D. na Onyango, P. (1991) *The Sociology of the African Family*. New York: Longman Publishers.
- Kezilahabi, E. (1971) *Rosa Mistika*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Kezilahabi, E. (1974) *Kichomi*. Nairobi: Heinemann Educational Books.
- MacNamara, E. na Karmen, A (Wah.) (1983) *Deviants: Victims or Victimisers?* Vol.7 Beverly Hills: SAGE Publications.
- Magare, W.A. (2002) *Uhakiki wa Tamthilia ya Amezidi kama kazi ya Kiubwege*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.
- Marx, K. (1939) *The German Ideology*. New York: International Publishers, Inc.
- Mbatia, A.M. (2001) *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing
- Mbatia, A.M. (2003) *A Critical Approach to Wamitila's Nguvu ya Sala katika Hekima Journal of the Humanities and Social Sciences* Juzuu la.2 na.1, 2003
- Mkangi, K. (2003) *Walenisi*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mogambi, H. (2003) *Mwongozo wa Walenisi*, Nairobi: World Link Press Publishers.
- Mohammed, S.A (2001) *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Mulokozi, M.M. na Kahigi, K.K. (1976) *Malenga wa Bara*. Nairobi: East Africa Literature Bureau.
- Munga, C.I. (1999) *Dhana ya Maisha katika Novela Mbili za Euphrase Kezilahabi: Nagona na Mzingile*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi. Haijachapishwa.
- Mutiso, K. (1996) *Archetypal Motifs in Swahili Islamic Poetry: Kasida ya Burudai*. Tasnifu ya Uzamifu (Ph.D) Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.
- Mwita, L.C. (2003) *Mwongozo wa Walenisi*. Nairobi: Africawide Network.

New Encyclopaedia Britannica (2003) Toleo la 15. Juzuu la 26. Chicago:

Encyclopaedia Britannica, Inc.

Novack, G. (mh.) (1960) *Existentialism versus Marxism: Conflicting Views on Humanism*.

New York: Dell Publishing Company, Inc.

Nyaundi, N. (2003) *Introduction to the Study of Religion*. Eldoret: Zapf Chancery Publishers.

Okullu, H. (1974) *Church and Politics in East Africa*. Toleo la 2001. Nairobi.

Uzima Press Ltd.

Okullu, H. (1984) *Church and State in Nation Building and Human Development*.

Toleo la 2003. Nairobi: Uzima Press Ltd.

Olali, T.M. (2004) *The Veneration of the Prophet: The Role of Kasida ya Hamziyyah During the Maulidi Festival of the Lamu Archipelago, Kenya*. Tasnifu ya Uzamifu (Ph.D) SOAS, London. Haijachapishwa.

Roubiczek, P. (1964) *Existentialism For and Against*. London: Cambridge University Press.

TUKI (1981) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Toleo la 1998. Nairobi: Oxford University Press

Wamitila, K.W. (1995) *Nguvu ya Sala*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Wamitila, K.W. (1998) *Towards Unlocking Katama Mkangi's Walenisi: A Case of a Parabolic Narrative?* Katika Jarida la *Kiswahili*. Juzuu la 61. Dar es Salaam: TUKI.

Wamitila K.W. (2003a) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi;

Phoenix Publishers.

Wamitila, K.W. (2003b) *Mwongozo wa Walenisi*. Nairobi: Sasa Sema Publications.

Warnock, M. (1970). *Existentialism*. London: Oxford University Press.

White, V. (1952) *God and the Unconscious*. London: Fontana Books.

Zaehner, R.C. (mha.) (1977) *The Concise Encyclopaedia of Living Faiths*. London: Hutchinson & Co.